SUPA JACKPOT
TZS. 1,139,859,317
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Waziri** Mkuu aagiza diaspora walinde heshima ya Tanzania nje

UKURASA 4



Shule zinapoona ahueni pale zulo la bweni linapoegezwa
Jihadhari usiwe kati ya 158,000 wanaokufa kila mwaka na dawa
Nipashe TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Wafugaji hapa ndipo ilipo nyama bora, ukuaji kasi mifugo na gharama nafuu
SAYANSI
NA CHRISTINA MWAKANGALE
Ndivyo nyuki alivyo mali kila kitu chake ni cha bei, thamani kubwa
• Anayo tiba ya uzee, anaumaliza ugumba sumu yake ghali hukaribia nusu milioni

UKURASA 11

# Nipashe
Jumanne Agosti 1, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • Na. 0581389
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# Nusu ya madaktari wafeli mtihani wao

• **Kati** ya 640 walioufanya mwaka huu, 366 waanguka; waibua hoja nane, Baraza laweka msimamo... *Endelea ukurasa 2*



> Uwezo wao darasani ni mdogo. Ni lazima warudie mtihani ili wafaulu, kazi wanayokwenda kuifanya inahusu uhai wa binadamu.
>
> **Dk. David Mzava, Msajili Baraza la Madaktari (MCT)**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### MKE NA MUME MBARONI TUHUMA ZA KUKATA KICHWA CHA KICHANGA

JESHI la Polisi Mkoa wa Kilimanjaro linawashikilia mume na mke, wakazi wa Kijiji cha Nayeme, wilayani Rombo kwa...

UKURASA WA 8

### CRDB YATANGAZA FAIDA YA BILIONI 265/- ROBO YA PILI YA MWAKA 2023



BENKI ya CRDB imeendeleza ufanisi kwa kupata faida ya Sh. bilioni 265 kabla ya kodi sawa na ongezeko la asilimia sita...

## Waziri aonya siasa kuingilia utendaji wa TANESCO

UKURASA 3



## Kinana, Lissu wajibizana vikali

UKURASA 5

MICHEZO MAYELE: NITARUDI YANGA SC UK.24
KATUNI UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akipokea tuzo maalumu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kutoka kwa Latifa Ismail ambaye ni Mhasibu wa Umoja wa Watanzania waishio St. Petersburg nchini Urusi alipozungumza nao kwenye hoteli ya Lotte nchini humo mwishoni mwa wiki. Tuzo hiyo ni ya kumpongeza Rais Samia kwa uongozi na utawala bora. Wa pili kushoto ni Katibu wa Umoja huo, Deogratias Kalulu. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Nusu ya madaktari wafeli mtihani wao

**Na Mwandishi Wetu**

KUIPATA leseni ya udaktari wa binadamu kuna kizingiti. Zaidi ya nusu ya madaktari tarajali waliofanya mtihani wa kuipata leseni hiyo mwaka huu wameanguka. Kati ya 640 walioufanya, 366 (asilimia 57) wamefeli.

Katika mazungumzo na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, mwakilishi wa madaktari tarajali hao, Baraka Shija, alidai zaidi ya wahitimu 300 wa fani ya udaktari waliofanya mtihani huo mwaka huu wamefeli.

Shija alidai kufeli kwao katika mtihani huo kumetokana na alichokiita urasimu ndani ya Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT), ikiwamo kuwataka wafanye mtihani wenye maswali 200 ndani ya saa tatu.

Katika ufafanuzi wake kwa Nipashe kuhusu suala hilo, Dk. David Mzava, Msajili MCT, alibainisha kuwa madaktari tarajali 640 walifanya mtihani wao Machi 22 mwaka huu. Kati yao, 274 (asilimia 43) walifaulu na 366 (asilimia 57) walifeli, akikiri kwamba idadi ya waliofanya vibaya ni kubwa.

Alitaja sababu kuu ya kufeli mtihani ni uwezo mdogo darasani kwa madaktari tarajali hao, akisisitiza ni lazima warudie kufanya mtihani ili kufaulu, kwa kuwa kazi wanayokwenda kuifanya inahusu uhai wa binadamu.

**MASWALI 200**

Kuhusu hoja ya mtihani kuwa na maswali 200, Dk. Mzava alisema hakuna uonevu katika hilo, akifafanua: "Kwa kawaida mtihani ni wa maswali 200 ambayo yamegawanywa katika mitihani miwili tofauti.

"Mtihani wa kwanza unahusu utabibu ambao unafanywa asubuhi, kisha wanapumzika. Baadaye wanafanya mtihani unaohusu mambo ya upasuaji. Kila mtihani ni maswali 100 na unafanywa kwa saa tatu. Hivyo, mtihani wa maswali 200, maana yake wanaufanya kwa saa sita."

Alisema utaratibu huo umewekwa kwa kuzingatia kwamba mitihani ya nyuma, madaktari walikuwa wanapewa maswali 150 kwa saa tatu, wakawa wanalalamika muda hautoshi.

"Baadaye baraza likaamua kwamba muda uongezwe, lakini pia likaongeza maswali kutoka 150 hadi kufikia 200, yakiwa yamegawanywa sehemu mbili ambayo ni 100 kwa mtihani wa asubuhi na 100 mengine kwa mtihani wa jioni, lakini wa kufanya maswali 200 ni saa sita," alifafanua.

Zinaporejewa hoja za madaktari tarajali, mwakilishi wao, Shija, anasema wamekuwa katika mazoezi ya vitendo (internship) katika hospitali kubwa za rufani nchini, wakisimamiwa madaktari bingwa kabla ya kufanya mtihani huo.

"Sisi madaktari tarajali tunashangazwa na kuumizwa na utaratibu wa Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT) kwa kadhia kubwa wanayotusababishia.

"Sisi tunaamini serikali ilikuwa na nia njema ilipoamua kutunga Sheria Na. 11 ya Mwaka 2017 ambayo ilipitishwa na Bunge letu, ikitaka kila mhitimu wa fani ya udaktari sharti apewe leseni baada ya kufanya mtihani wa MCT.

"Bahati mbaya, chombo hiki hakijaweza kujua kifanye kazi ipi na kwa wakati upi ili kiweze kulisaidia taifa lipate madaktari bora na siyo bora madaktari.

"Tunachokipinga ni hii idadi kubwa ya wanaofeli mtihani huu. Tunaomba mtihani huu usahihishwe upya na wasimamizi wa nje ya MCT," alisema.

Shija alidai MCT haina uwazo katika alama za ufaulu na uendeshaji mzima wa mtihani na matokeo utakaomfanya mtu ajue amefeli idara ipi hata baada ya kukata rufani.

Alisema kuna haja serikali iingilie kati kufuatilia alichokiita upungufu wa MCT na itumie dhamana yake kuwawezesha madaktari tarajali wapate leseni ili washiriki katika ujenzi wa taifa.

Shija pia alisema wanashauri vyuo vya udaktari viwe chini ya Wizara ya Afya badala ya Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) ili visimamiwe vizuri zaidi katika kutoa wataalamu wazuri wa kada hiyo.

Akijibu hoja ya kutokuwapo uwazi katika matokeo ya mtihani wa udaktari, Dk. Msava alisema: "Ni muhimu daktari awe ameiva. Hakuna urasimu wa kutooneshwa matokeo au wamefeli wapi. Hayo yote hayana ukweli. Katika kazi yetu tunazingatia sana huduma, tunataka daktari akatoe huduma nzuri.

"Daktari kutaka kuoneshwa matokeo au ni wapi daktari amekosea, halina umuhimu kuliko kwenda kutoa huduma bora kwa wananchi, hivyo ukiona daktari amefeli, ujue amefeli, si vinginevyo."

## Digitali yaongeza uhai wa UTT AMIS

**Frank Monyo na Halfan Chusi**

TAASISI ya UTT AMIS imejivunia mafanikio ya kiutendaji waliyoyapata kwa kipindi cha miaka minne kwa mifuko ya taasisi hiyo kukua kutoka Sh. bilioni 496- hadi trilioni 1.52 kutokana na matumizi ya kidigitali.

Akizungumza katika mkutano na wahariri na wanahabari uliofanyika jana mkoani Dar es Salaam kuhusu uendeshaji wa mfuko huo, Mkurugenzi Mtendaji wa UTT AMIS, Simon Migangala, alisema mfuko huo umepata matokeo chanya katika kipindi cha miaka minne na wastani wa ukuaji wake kwa mwaka ulikuwa asilimia 50.

"Kwa kutumia mifuko hii mwekezaji mdogo akiwa na kiasi chochote cha fedha anaweza kuwekeza na UTT AMIS katika masoko ya fedha na faida inayopatikana katika masoko hayo inarejeshwa kwa wawekezaji hivyo inasaidia mwekezaji mdogo kupata faida kubwa kama anayopata mwekezaji mkubwa," alisema.

Alisema, sababu nyingine iliyosababisha ukuaji huo kwa mujibu wa Migangala ni kipindi cha mlipuko wa Uviko-19.

"Japo kipindi cha Covid-19 tulipoteza ndugu zetu wengi, lakini ndiyo kipindi ambacho watu wengi walijiunga nasi kwa ajili ya kuwekeza katika mifuko yetu," alisema na kuongeza;

"Wakati wa Covid-19 watu wengi waliamua kuwekeza kwenye mfuko wetu kwa sababu hawakutaka akiba yao ibaki bila kazi, ambayo ilikuwa faida kwa UTT-AMIS,"

Alisema mwaka jana, mfuko huo uliongeza thamani ya mali zake hadi kufikia Sh. bilioni 996 kutoka Sh. bilioni 619 mwaka uliopita, akihusisha utendaji kazi na sera nzuri za uwekezaji. Pia katika kipindi cha miaka minne, mfuko umeendelea kuvutia wawekezaji wapya hasa kutokana na kukua kwa imani na uelewa wa wananchi kuhusu faida za kuwekeza katika miradi ya uwekezaji wa pamoja.

Alisema ukuaji huo mkubwa pia ulichangia na kuimarika kwa uelewa wa wananchi kuhusu faida za mfuko, utendaji mzuri wa masoko ya fedha, maamuzi mazuri ya uwekezaji kutoka kwa meneja na kuungwa mkono na wadau mbalimbali.

Meneja Uhusiano wa Umma na Masoko wa UTT-AMIS, Daudi Mbaga, alisema zamani mfuko huo ulikuwa na akaunti 500 pekee, lakini kwa sasa zimepanda na kufikia zaidi ya 2,000.

Miongoni mwa sababu za kuongezeka kwa akaunti ni pamoja na kuboreshwa kwa mifumo ambayo wawekezaji wanaweza kuwekeza kwa kutumia majukwaa ya fedha kwa njia ya simu kinyume na hapo awali ambapo walitakiwa kutembelea mfuko huo.

Alisema mwamko wa umma umeongezeka hadi asilimia 20 katika maeneo ya mijini akisema hii imeonekana katika ongezeko la uwekezaji.

Mbaga, aliongeza kuwa katika kufanikisha UTT AMIS, inaendelea kupiga hatua wamekuwa wakitoa elimu ya uwekezaji katika ngazi mbalimbali, ikiwamo vyuoni na sasa wana mkakati wa kuhakikisha kuwa kwenye mitaala ya elimu linaongezwa somo hilo.

# Makamba: TANESCO isiingizwe kwenye siasa

**Na Jenifer Gilla**



WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amewataka wanasiasa kuliacha Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), litekeleze majukumu yake bila kuliingilia kwa kuwa inashusha ufanisi wa watendaji.

Aidha, amewataka wanasiasa wanaoona kuna upungufu kwenye shirika hilo wamfuate waziri moja kwa moja badala ya kuwaingilia wafanyakazi kwa kuwa anaweza kumudu changamoto za siasa.

Akizindua Taarifa ya Mwaka wa Fedha (2020/2021) na Mpango Mkakati wa Shirika wa miaka kumi jana jijini Dar es Salaam, Makamba alisema shirika hilo litaendelea kufanya kazi kwa uwazi ikiwamo kutangaza mikakati yake ili lihukumiwe litakaposhindwa kutekeleza mipango hiyo kwa kuwa lengo ni kutoa huduma stahiki kwa wateja wake.

Alisema ni muhimu TANESCO ikaweka wazi changamoto inazokabiliana nazo na maboresho yanayoendelea kwa wateja wake, ili wazifahamu na wao wafanye kazi kwa uhuru kuliko kujaribu kuficha kwa namna yoyote.

"Msiwazongezonge na siasa, njooni kwetu sisi siasa tunaziweza, kwa sababu inawasumbua, wanaanza kuulizana oh! Mtandaoni wameandika nini, sisi tunataka wafanyakazi wa TANESCO, bodi, menejimenti wafanye kazi kwa utulivu," alisisitiza Waziri Makamba.

Alisema umeme ni kichocheo kikuu cha maendeleo ya nchi kutokana na kuwezesha utekelezaji wa shughuli katika sekta nyingi ikiwamo kilimo, afya na mifugo.

Waziri Makamba alihakikisha kwa kulitambua hilo serikali itaendelea kulishika mkono ili litimize malengo yake na hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan aliridhia deni la Sh. trilioni 2.4 lililokuwa linadaiwa libadilishwe kuwa mtaji kwa shirika katika uwekezaji, jambo ambalo halijawahi kutokea.

Alisema pamoja na mafanikio makubwa shirika iliyoyapata bado lina kazi kubwa ya kufanya ili kutoa huduma inayostahiki kwa Watanzania, ikiwamo kuboresha miundombinu itakayowafikia wateja wake kwa urahisi.

Akiwasilisha Mpango Mkakati wa miaka 10 wa Shirika hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, alitaja vipaumbele vinane vya shirika kutimiza malengo yake ikiwamo kuongeza kasi ya kutatua changamoto za wateja wao.

Vipaumbele hivyo ni kukuza ujuzi wa wafanyakazi wake, kuweka usimamizi madhubuti na mabadiliko ya kiutendaji ili kuwe na uhuru na ushirikishwaji katika utendaji kazi na kukuza ufanisi kwa watendaji wake.

Kuendeleza utunzaji mazingira wakati wa utekelezaji wa miradi yao na kuwekeza kwenye nishati mbadala ikiwamo umeme wa maji.

Vilevile, alisema shirika litakuza teknolojia ya umeme ili kuwafikia Watanzania wengi na kufanya biashara na uwekezaji kwa ajili ya kuliingizia mapato.

Kwa mujibu wa Chande, kabla ya uandaaji wa mpango huo wa muda mrefu, waliandaa wa muda mfupi wa 2021/22 ambao ulilenga zaidi kutatua kiu ya changamoto za umeme wanazopitia wateja wao.

"Ili kutimiza lengo hilo shirika lilikusanya maoni kutoka sehemu mbalimbali, ikiwamo kwa wateja ili kujua changamoto wanazokabiliana nazo na namna ya kuzitatua," alisema.

Katika utekelezaji wa mpango huo wa mwaka mmoja, Shirika lilifanikiwa kuongeza ushiriki wa wafanyakazi wao katika kazi kutoka asilimia 49 na sasa ni asilimia 58, huku ushirikishwaji wa wanawake katika ngazi za maamuzi umeongezeka kwa asilimia tatu.

Alisema katika kipindi cha mwaka mmoja wameunganishia umeme wateja 54,366 jambo ambalo halijawahi kutokea tangu kuanzishwa kwa Shirika hilo.

Pia, wameongeza mapato kutoka Sh. trilioni 2.60 hadi Sh. trilioni 2.826 pamoja na kupunguza matumizi kutoka Sh. trilioni 2.18 hadi Sh. trilioni 2.076.

Kuhusu upotevu wa umeme, alisema umepungua kutoka asilimia 15 hadi 14.5 na utayari wa mashine kuzalisha umeme umeongezeka kufikia asilimia 88 kuzidi lengo ambalo ni asilimia 85.

Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO, Omari Issa, alisema deni lililosamehewa na serikali na kugeuzwa kuwa hisa limeisaidia shirika hilo kuwa na hesabu safi na sasa wamesimama vizuri kutekeleza majukumu yake.

Hata hivyo, alisema shirika linakabiliwa na changamoto ya rasilimaliwatu na katika kuitatua changamoto hiyo wamepeleka wafanyakazi katika vyuo vya nje ya nchi, ili kupata watu wenye weledi na uadilifu wa kuliongoza vyema shirika hilo miaka ijayo.

"Kitakaporudi hicho kikundi, kikundi kingine kitaenda na tunapeleka vikundi katika nchi na vyuo mbalimbali ili tuweze kuwaandaa na kuliongoza hili Shirika katika hiyo miaka kumi na kuendelea," alisema Omari.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Judith Kapinga, alisema mpango makakati wa shirika hilo ni dira ya kufikia malengo ya maendeleo ya muda mrefu katika sekta ya umeme.

Alisema kamati hiyo inaendelea kusimamia na kutoa ushauri ili kuhakikisha shirika hilo linaendelea kuwa taasisi inayotoa huduma bora na endelevu kwa manufaa ya taifa.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONYESHA NIA: UTOAJI WA HUDUMA ZA MAFUTA KWA MAGARI MDOGO NA VIFAA VINGINE KWENYE NJIA YA MKUZA WA BOMBA LA MAFUTA KATIKA MRADI WA EACOP. KUMBUKUMBU Na. 00000315

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD"), inaalika kampuni yenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma ya mafuta kwa ajili ya magari madogo na vifaa vingine kwenye njia ya Mkuza nchini Tanzania.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili, kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale, katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
EACOP Ltd, ina Magari/mitambo, kadhaa ambayo hufanya kazi mbalimbali kwenye maeneo yashughuli za EACOP na hivyo magari hayo yatasambazwa kote chini Tanzania. Magari na mitambo hiyo yote itahitaji kuwekewa mafuta katika vituo mbalimbali ndani na nje ya maeneo ya uendeshaji wa mradi. Kwa hiyo, EACOP Ltd inahitaji watoa huduma mbalimbali kueleza nia yao ya kutoa huduma za mafuta kwa Kampuni ikiwa ni pamoja na usambazaji wa:

- Mafuta ya Petroli na Dezeli.
- Huduma nyingine zinazohusiana na magari na mitambo midogo ikijumuisha, huduma ya kuosha magari katika vituo hivyo vya mafuta, na/au uwezo wa kutoa huduma ya Oili, grisi, na huduma za ndogo zisizo za kimakanika.
- Kwa sasa Mradi unapitia katika mikoa ya Bukoba, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga hususan katika wilaya za Muheza, Handeni, Kilindi DC, Kibirashi, Kiteto (Kibaya), Hanang, Chemba, Igunga, Kagongwa, Bukombe (Ushirombo), Chato, Muleba, Misenyi (Mutukula), Kyaka kwa hiyo mtoa huduma lazima awe na kutuo cha mafuta katika maeneo hayo na Tanzania kwa Ujumla.
- Inapendekezwa sana kituo cha mafuta kiwe na Kadi za usumaku za kukwaruza au zenye msimbo na nywira au namba za siri za kutolea mafuta.

**VIGEZO MUHIMU:**
**Kampuni au taasisi zinazoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo.**

- Uthibitisho wa kusajiliwa kama muuzaji wa mafuta/Kituo cha mafuta/Kampuni ya mafuta kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Tanzania.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na mamlaka husika ikiwa ni pamoja na OSHA, EWURA, TBS etc.
- Uthibitisho wa uzoefu wa kufanya kazi katika miradi yenye mahitaji makubwa ya mafuta ikijumuisha orodha ya kampuni 5 unazofanya nayo kazi kwa sasa au yaliyopita.
- Leseni ya Biashara.
- Cheti cha usajili toka BRELA (ambatanisha cheti).
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlakaya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha mlipa kodi cha mwaka wahivi karibuni.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamesajiliwa kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia.
- Kukidhi vigezo na Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya ndani.
- Ushahidi wa sera na Mifumo ya Usimamizi wa shirika la HSE, utaratibu na mchakato kwa mujibu wa viwango vinavyotumika vya ndani na Viwanda kwa kazi zinazofanana.
- Uthibitisha wa wasifu wa wafanyakazi mhimu watakaohusika katika kutoa huduma za mradi ikijumuisha vyeti vyao, kiwango cha elimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma husika.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa za fedha ya miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho wa kupiga vita rushwa, ufisadi, kwa kuzingatia Haki za Binandamu.

Kampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu zinakaribishwa kutuma maombi pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com**, (ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb**). Maombi yatumwe kabla au mnamo tarehe **15th Agosti 2023 saa 11 jioni** saa za Afrika Mashariki. Kichwa cha Barua pepe kiwe **REQ-00000195 - kutoa huduma ya Bima ya Dhima kwa wakurugenzi na Mafisa wa Mradi wa EACOP**. Maombi yote ya kuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.
Maombi yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na kampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini kampuni zitakazojumuishwa kwenye orodha ya (kampuni) ya awali yaliyokidhi vigezo. Kampuni zilizofuzu hatua za awali pekee ndiyo yatakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

# Mke na mume mbaroni tuhuma za kukata kichwa cha kichanga

**Na Mary Mosha,** ROMBO

JESHI la Polisi Mkoa wa Kilimanjaro linawashikilia mume na mke, wakazi wa Kijiji cha Nayeme, wilayani Rombo kwa tuhuma za kuua kichanga anayekadiriwa kuwa na umri wa miezi miwili au mitatu kwa kumchinja na kumtenganisha kichwa na kiwiliwili kisha kuzika kichwa na kuficha kiwiliwili katikati ya magodoro.

Akidhibitisha tukio hilo jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa, alisema Melania Tarimo (32) ambaye ni mama mzazi wa kichanga hicho, kwa kushirikiana na Priscus Daniel, maarufu Mtivei, aliyekuwa anaishi naye - baba wa mtoto huyo, wanadaiwa kufanya unyama huo Mei mwaka huu.

"Wananchi pamoja na uongozi wa kitongoji walimjengea shaka mama huyo baada ya kutomwona mtoto wake mchanga. Walianza kudadisi bila mafanikio kisha wakatoa taarifa katika kituo cha polisi. Tulianza uchunguzi na Julai 6 mwaka huu tuliwatia mbaroni wawili hao ambao ni mume na mke.

Kamanda alisema walifanya uchunguzi na kubaini mtoto huyo alishafariki dunia na kuzikwa bila kushirikisha viongozi wa kijiji, ndugu, majirani wala mmiliki wa eneo alikozikwa.

"Uchunguzi wa awali ulionyesha mtoto huyo ni wa kike. Mauaji hayo yanadaiwa kufanyika na baada ya kumuua walizika kichwa katika eneo la nyumba hiyo na kiwiliwili kilikutwa kimefichwa katikati ya magodoro yaliyokuwapo katika chumba walichokuwa wakiishi. "Nyumba waliyokuwa wakiishi, mmiliki wake yuko Arusha na wao waliwekwa hapo kwa ajili ya kufanya kazi. Tumefukua eneo tuliloonyeshwa, tumefukua na kukuta mabaki ya fuvu la kichwa na vipande vya nguo," alisema.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kitakura, Eva Moshi, alimwambia mwandishi wa habari hizi kuwa yeye ni miongoni mwa waliobaini tukio hilo baada ya kusikia minong'ono miongoni mwa wananchi wake kuwa Melania hajaonekana na mtoto kwa muda licha ya kujulikana kujifungua. Alianza kufuatilia ili kupata ukweli huo.

"Niliamua kwenda kuonana na mama huyo na kutaka kupata taarifa zaidi za mtoto, hakuwa na majibu yanayojitosheleza. Mwanzoni alisema yuko nyumbani. Tulipofika nyumbani anapoishi akasema yuko katika kituo cha watoto yatima cha Ngaleku, nilipomtaka twende kituoni huko alikataa.

"Aliniambia mtoto aliugua ghafla na kumkimbiza hospitalini na kupata matibabu na kurudi nyumbani, jioni alizidiwa na kufariki dunia na kwamba walimzika yeye na mumewe. Alinitia shaka nikaenda kutoa taarifa kituo cha polisi na ndipo uchunguzi wa kina ulipoanza.

"Baada ya polisi kufika, mama huyo alieleza ukweli juu ya tukio hilo na kichwa cha kichanga hicho kilikutwa kimefukiwa ndani ya geti la nyumba ya bosi wake na kiwiliwili kilikutwa kimefunikwa katikati ya godoro," alidai.

Inadaiwa kuwa baada ya Melania kupata mwanamume mwingine waliyeshirikiana kufanya mauaji, walikuwa wakigombana kuhusu mtoto huyo na kuna wakati walimtupa.

"Mara kadhaa wamekuwa wakirushiana mtoto, mwanamume alikuwa akimwambia si wake ndiyo maana wakaamua kumuua ili wazae mwingine," alidai kiongozi huyo wa kitongoji.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Deogratius Maruba, alisema mwili wa mtoto huyo ukiwa umeharibika, ulipokewa na kuhifadhiwa katika Kituo cha Afya Karume na walitoa taarifa Kituo cha Polisi Karume kwa hatua zingine za kisheria.

"Julai 8, mwaka huu katika Kituo chetu cha Afya Karume tulipokea mwili wa mtoto anayekadiriwa kuwa na umri wa miezi miwili mpaka mitatu ambao ulikuwa umeharibika," alisema.

Gaudenisia Shirika (89), mkazi wa Ibukoni, wilayani Rombo, akizungumza na mwandishi kuhusu tukio hilo, alisema:

"Ni la ukatili. Mimi siridhiki nalo na ninaomba hatua za kisheria zichukulie zaidi juu ya vijana ambao wafanya matukio kama haya nchini, vijana waache kurukaruka na ninashauri wabunge watunge sheria endapo mtu atabainika kumpa mimba mtu awe na jukumu la kumuoa, akikaidi jela miaka 30.

"Hii itasaidia watu kupunguza ukatili. Enyi wanawake, mtoto ni mali yako. Ikiwa mwanamume amemkataa, usikubali kuua, pambana, Mungu atakusaidia.

"Wazazi tusimamie malezi ya watoto ili wamrudie Mungu na kuacha matumizi ya dawa za kulevya yanayopelekea watu kukosa uamuzi sahihi."




Wafanyabiashara wadogo wakitandaza biashara zao stendi ya mabasi Kimara Mwisho licha ya kuwapo kwa tangazo la halmashauri la kuwakataza kufanya biashara katika eneo hilo kama walivyokutwa Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## PM: Diaspora tunzeni heshima ya Tanzania

**Na Mwandishi Maalum**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewataka wanadiaspora wa Tanzania wazingatie sheria za nchi wanazoishi ili waendelee kutunza heshima ya nchi yao.

Alitoa wito huo jana alipozungumza na Watanzania wanaoishi St. Petersburg, Urusi ambako alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika mkutano wa pili wa kilele baina ya wakuu wa nchi na Serikali kutoka mataifa ya Afrika na Urusi.

"Baadhi yenu mko hapa mnatafuta fursa, na wengine wengi wapo hapa kwa masomo. Zingatieni sheria za nchi hii, tunzeni heshima ya Tanzania. Teteeni Taifa la Tanzania, zungumzieni fursa zilizoko nyumbani," alihimiza Waziri Mkuu.

Alisema katika baadhi ya vikao vyake na wawekezaji wa Kirusi, hakupata shida ya mkalimani kwa kuwa walikuwa na mtu wao ambaye anatafsiri moja kwa moja kutoka Kirusi kwenda Kiswahili na Kiswahili kwenda Kirusi.

"Lakini na sisi ubalozini kwetu tuna Ofisa Uchumi ambaye alitusaidia kutafsiri Kiswahili kwenda Kirusi kwenye baadhi ya vikao. Tena aliongea kwa ufasaha zaidi. Tusiache fursa hii itupite," aliwasisitiza.

Akimkaribisha Waziri Mkuu kuzungumza na washiriki wa kikao hicho, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Mbarouk alisema mbali na kudumisha uhusiano wa kirafiki na kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi zingine, serikali imeendelea kuratibu masuala ya diaspora.

"Mfumo huo uliotengenezwa na wataalamu wazawa utasaidia kurahisisha usajili wa diaspora wenye asili ya Tanzania pamoja na wanafunzi."

Akisoma risala yao, Mwenyekiti wa Diaspora katika Shirikisho la Urusi na Nchi Huru za Jumuiya ya Madola (CIS), Pascal Gura, alisema jumuiya yao (TADRU- CIS), ina wanachama zaidi ya 200 walioko sehemu tofauti za nchi hiyo.

Alisema kwa sasa wanadiaspora hao wanakabiliwa na changamoto ya mifumo ya kifedha kutokana na vikwazo vya kiuchumi.

Wanadiaspora hao pia walimkabidhi Waziri Mkuu tuzo ya Rais Samia kutambua juhudi zake katika kuwaletea wananchi maendeleo.

# Waziri apongeza kuanzishwa kanzidata ya maarifa ya AZAKI

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesifu kuanzishwa Kanzidata ya Maarifa kwa ajili ya Asasi za Kiraia nchini, akisema kutakuwa na faida kubwa kwa wizara na nchi kwa ujumla.

Katika hotuba yake ya uzinduzi wa kanzidata hiyo wakati wa hafla iliyofanyika Kinondoni, Dar es Salaam jana, Waziri Dorothy alisema amefurahi kuona asasi zitaungana pamoja na wadau wa maendeleo katika kupeana uzoefu katika utendaji kazi kupitia kanzidata hiyo.

"Ni dhahiri kuwa mabadiliko chanya yatakuwa endelevu kupitia azaki kubadilishana taarifa na kujifunza tulikotokea na kujipanga kwa yajayo. Wadau wataweza kuhimiza maendeleo na kutengeneza mustakabali.

"Nimefurahi kuona wengine ambao ni wadogo ndiyo kwanza wanasajiliwa wataweza kujifunza nini kinafanyika kwa wenzao na kuomba msaada na kupata usaidizi papohapo," alisema.

Dk. Dorothy alisema kutumia takwimu katika kazi za asasi ni muhimu, hasa katika kufanya ushawishi. Ni takwami zitakazoisaidia serikali kurekebisha mahali patakapoonekana hapakaa sawa.

"Na hii inawezekana tu pale tukiwa na kanzidata ili kupata taarifa kwa urahisi kati ya serikali na wadau wote. Mheshimiwa Rais amekuwa akihimiza ushirikiano kati ya serikali na wadau wa maendeleo," alisema.

Aliongeza: "Utafiti unaonesha bado kuna changamoto kubwa kwa wadau wa azaki kutumia takwimu katika shughuli zao za uchechemuzi, hivyo kuna umuhimu kuendelea kuhakikisha wanaweza kutumia takwimu.

"Nimefurahi kusikia kuwa baada ya uzinduzi huo kutakuwa na mafunzo yatakayofanyika katika mikoa ya Dodoma na Arusha ambapo wataalamu waliounda mfumo watafundisha wadau kutumia mfumo."

Awali, akimkaribisha waziri huyo, Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Vickness Mayao, alisema kanzidata hiyo itasaidia kuongeza ufanisi katika utendaji wa mashirika.

"Kupitia kanziadata hii tunaweza kupunguza mlundikano wa watu katika eneo moja na hata kutanua huduma kufika mbali zaidi. Tujitahidi sana data tutakazoziweka humo kwa sababu serikali itazitumia, ziwe zimepitishwa na vyombo vinavyohusika kama NBS (Ofisi ya Taifa ya Takwimu)," aliagiza.

Mjumbe wa Bodi ya Umoja wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania (TANGO), Ludovick Utouh, alihimiza kanzidata hiyo itumiwe kwa maendeleo ya asasi na nchi kwa ujumla.

Aliutaja uzinduzi huo ni hatua kubwa kuelekea mashirika hayo kujisimamaia na kujiongoza ili kufikia malengo endelevu katika kutekeleza vipaumbele vya nchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Freedom House, Daniel Lema, aliahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa asasi katika kutekeleza majukumu yake.

Kupitia kanzidata hizo, wadau wanaweza kupakua taarifa mbalimbali za utekelezaji wa shughuli za asasi katika mikoa mbalimbali nchini.

# Kinana, Lissu wajibizana vikali

**Na Waandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana, amesema wakitetereka na kukubali kupotoshwa, watapoteza malengo huku akionyesha kukerwa na alichokiita kashfa, kejeli na matusi yanayotolewa na Vyama vya Upinzani dhidi ya Rais.

Katika mkutano na wananchi jana mkoani Tabora, Kinana alisema ajenda za wenzao (upinzani) ni za msimu lakini za kwao (CCM) ni za kudumu. Wana mkataba na wananchi kupitia ilani, malengo na ahadi walizozitoa, huku akieleza hatua mbalimbali Rais Samia Suluhu Hassan alizozitumia kuimarisha demokrasia nchini.

Kinana alisema Rais Samia alianza utaratibu wa kukutana na wapinzani wote nchi nzima kupitia Baraza la Vyama vya Siasa ili kuzungumzia hali ya siasa, demokrasia na namna ya kupata Katiba nzuri ambayo itatoa nafasi ya uchaguzi huru na wa haki, tume nzuri ya uchaguzi na sheria itakayosimamia vyama vya siasa.

"Bahati mbaya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) walikataa kwenda katika shughuli hiyo. Hawakwenda katika Baraza la Vyama na kwenye Kituo cha Demokrasia walikataa. Wengine wote walikubali. Tunaendelea, hatukuwalazimisha mkatae.

"Lakini Rais akasema 'hapana! Hawa nao wana hasira wamekataa kujiunga na wenzao kujadili mambo ya msingi ya Taifa letu, lazima tuwasikilize'.

Alipoamua hivyo, kuna watu ndani ya CCM hata nje hawakupenda huo uamuzi wa Rais 'kwanini awape fursa ya pekee CHADEMA?'" Kinana alidai.

Alisema Rais aliwapa fursa ya kuwasikiliza ili ajue ni kwanini walikataa kushirikiana na vyama vingine na kuisikiliza serikali. Mei 2022 Rais aliwaalika CHADEMA katika kikao ambacho mwenyekiti alikuwa yeye.

Alisema Rais Samia alitoa wito kwa CHADEMA kwamba wajenge nchi kwa amani na umoja, akieleza kuwa kamati ya watu 10 iliundwa ikihusisha watano wa CCM na watano wa CHADEMA.

"Leo (jana) ninayasema haya kwa sababu mimi ni mwenyekiti kwa upande wa CCM katika suala hili la majadiliano. Wenzetu walikuja na hoja 15 na nyingi zilikuwa na madai. Kwa upande wa serikali, sisi hatukuwa na hata moja.

"Tulianza kuwasikiliza kila tukifikia hatua fulani tunapeleka taarifa kwa Rais. Kwanza, walisema kuna wafungwa wako jela waliofungwa kipindi cha uchaguzi, walikuwa zaidi ya 400 wakaomba waachiwe na waliachiwa," alisema Kinana.

Aliendelea kueleza kuwa CHADEMA pia walitaka serikali itoe kauli ya kuwahakikishia usalama wote waliokuwa nje ya nchi akiwamo Tundu Lissu, waambiwe warudi na wahakikishiwe usalama wao.

Kinana alisema kuwa kupitia Baraza la Vyama, vyama vyote vya upinzani vilimwomba Rais Samia kuondoa katazo la mikutano ya hadhara ombi ambalo lilikubaliwa, huku Rais akieleza kuwa ana matumaini kwamba kufunguliwa kwa mikutano ya hadhara kutatoa fursa ya kwenda kujadili yenye manufaa kwa Taifa.

"Rais alikuwa na matumaini kwamba itatoa fursa kwa watu kujadili na kuzungumzia sera, kujenga hoja na kuepuka mambo ambayo yatavunja umoja na mshikamano wa taifa, mikutano imeanza lakini baadhi yao badala ya kujenga hoja wanaleta vioja," alidai Kinana.

"Wanahoji baadhi ya hoja na vioja wanasingizia watu vitu havipo na uongo, sio jambo jema hata kidogo. Hawawezi tuhumu na kumsema vibaya mwenye mamlaka, lakini ametulia amekaa kimya anavumilia. Si kwamba hawasikii, anawasikia sana lakini ninadhani ana uvumilivu kuliko wao.

"Ana busara kuliko wao na anajua mamlaka aliyonayo akiamua kuyatumia, kuna watu wanaweza kuumia. Sasa mimi ninataka niwasihi... hatukatai mtoe hoja, na kusema yale mnayotaka kusema lakini semeni kiungwana.

"Zungumzeni kwa busara, jengeni hoja, kusema Rais ana akili za matope ni anauza Bandari, wewe sema mkataba huu haujakaa vizuri unaeleweka! Toa hoja kwanini haujakaa vizuri upande wa pili walisema umekaa vizuri, sema.

"Lakini ukisema mkataba huu hata kichaa hawezi kuukubali, maana nyingine ni kwamba unatuambia sisi sote ni vichaa, si sawa hata kidogo, nitumie fursa hii kusihi unaweza kupeleka ujumbe mzuri kwa njia ya kistaarabu na kujenga hoja na ujumbe wako ukaeleweka," alisema Kinana.

**LISSU AMJIBU**

Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, katika kile kilichoonekana kujibu hoja hizo za Kinana, alisema jana kuwa maridhiano yanayofanyika baina ya viongozi wa CCM na chama chao siyo sababu ya kuwafanya wanyamaze pale wanapoona kuna mambo hayaendi vizuri nchini.

Katika mkutano wa hadhara Namonge, mkoani Kagera jana, Lissu alisema "Kinana amesema 'CHADEMA hawana shukrani, walikuwa na kesi kibao tumewaachilia, badala ya kushukuru, wanatutukana'. Sasa walitaka tuwashukuru kwa kutufungulia kesi za uongo? "Kinana anasema 'tumewapa ruzuku yao'. Sasa kama ni ruzuku yao mmewapaje? Isingekuwa yetu, wangesema tumewapa ruzuku isiyokuwa yao... lakini anasema tumewapa ruzuku yao ya muda wote... ni kweli si ilikuwa yetu!"

Lissu alisema yale ambayo yametekelezwa na serikali ambayo ni miongoni mwa hoja zilizowasilishwa na CHADEMA kwenye vikao vya maridhiano yapo kisheria na siyo hongo kwao.

"Sheria za Tanzania zinasema ni halali kwa vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara, hamkutupa fadhila, mliondoa haramu mliyoileta wenyewe... hatuwezi tukawashukuru kwa kuondoa haramu mliyoileta wenyewe," alisema Lissu.

Aliongeza: "Kama mlifikiri mnatuachia kama hongo, hatuhongeki, haipo hiyo! Kinana anasema 'tumewaachia wafanye mikutano...' Tumefanya mikutano ya hadhara kwa zaidi ya miaka 30 ya mfumo wa vyama vingi vya siasa, lakini ilipigwa marufuku kiharamu... mlichofanya hamjatupa chochote ambacho sheria za Tanzania zimasema siyo halali yetu.

"Sisi ukitufunga bure tutakusema na ukituachia bure tutakusema... ukiiba tutakusema mchana kweupe... sisi hatuhongeki. Na kazi ya mikutano ya hadhara ni kueleza wananchi ubovu wa serikali iliyopo madarakani na chama kilichoko madarakani. Ndiyo kazi yetu. Tutakuwa na haja gani ya kufanya mikutano kama tutakuwa tunakwenda kuisifu hata pale ambapo mambo hayaendi vizuri?" alihoji.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Fursa ya watalii wanaoingia nchini isichezewe

**WAZIRI** wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amewakemea baadhi ya wafanyakazi wa hoteli wanaotoa lugha mbaya kwa watalii.

Baadhi ya wafanyakazi hao wanadaiwa kutumia lugha hiyo wakati wakiwahudumia watalii.

Baraka ya kupata watalii wanaoingia nchini kuja kuangalia vivutio isiharibiwe na watu wachache kwa sababu tu ya kushindwa kutoa lugha ya staha kwa wageni.

Nchi jirani zinatafuta fursa hiyo zinakosa na hata kuthubutu kutangaza vivutio vya Tanzania kuwa vinapatikana nchini kwao.

Rais Samia Suluhu Hassan, amefanyakazi kubwa ya kuutangaza utalii wa Tanzania mpaka wageni sasa wanamiminika kuja kuangalia vivutio hivyo.

Kazi hiyo ya Rais na nguvu aliyoitumia, isiharibiwe na watu wasiokuwa na uzalendo wa kuipenda nchi yao na kuitangazia mema.

Akiwa jijini Arusha wakati akifunga mafunzo ya kukuza ujuzi kwa wafanyakazi wa hoteli, yalioratibiwa na Wizara ya Utalii, Prof. Ndalichako, aliwaonya baadhi ya wafanyakazi wa hotelini kwa kusema kuwa katika utafiti walioufanya katika hoteli 35 imebainika kuwa utoaji wa huduma usioridhisha kwa wateja, lugha mbaya, matumizi ya simu ya kiganjani wakati mteja anasubiri huduma na ukosefu wa ujuzi wa kuhudumia wateja.

Fikiria, mgeni ametoka nchini kwake mbali kuja nchini kwako halafu anapata mapokezi mabaya, mtu wa mapokezi anaongea na simu tena wakati mwingine siyo ya kazi anapiga stori na rafiki.

Kwa hili la kutumia simu wakati mteja akihitaji huduma, liko kila sehemu ya kazi. Hata hospitali mtu anapokwenda kupata matibabu, baadhi ya wahudumu wa afya badala ya kumsikiliza mgonjwa, wanaongea na simu bila kujali ana tatizo gani.

Wafanyakazi wa hoteli wanatakiwa kuwa na ujuzi wa kutoa huduma bora ili kuvutia watalii kutamani kurejea Tanzania wanaporejea kwao.

Ni lazima Watanzania wajitafakari katika utoaji wa huduma kwa wageni kwa sababu tatizo hili linaonekana ni la kawaida la kutowajali wateja.

Hata kwa upande wa usafi wa vyumba katika baadhi ya hoteli hauridhishi. Mgeni anakaribishwa kwenye chumba na kukutana na harufu ya uvundo.

Vyoo havisafishwi vizuri mpaka vinageuka rangi na kuwa kahawia. Kwa kweli hili linahitajika kufanyiwa kazi kubwa ili kubadilisha hali hii.

Kwa upande wa chakula pia, mteja anaweza kuagiza chakula anachokitaka kwa matakwa yake, lakini ataletewa tofauti na anapohoji, hupata majibu yanayoudhi.

Waziri mwenye dhamana na utalii anasema serikali imeanzisha programu kusaidia kukuza ujuzi kwa wafanyakazi wa hoteli ambao wengi ni vijana na wameingia katika ajira bila kuwa na ujuzi stahiki.

"Hatuwezi kuwaacha kuendelea kufanya kazi hii, bila ujuzi na ndiyo maana tumeamua kutengeneza mifumo ya kukuza ujuzi kwenu, ili mtoe huduma stahiki kwa wageni wetu."

Pia alisema serikali baada ya kutoa mafunzo hayo, watafuatilia kuona mafanikio yake na kuboresha pale panapohitajika.

Programu ya kukuza ujuzi kwa wafanyakazi wa hoteli imeanzia Arusha kwa kuwa ni kitovu cha utalii.

"Tulibaini katika utafiti wetu wageni wengi hasa wanaotoka nje ya nchi hawapendi kufikia hoteli za kati sababu ya huduma zinazotolewa huko sio stahiki."

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Changamkieni tenda, Samia Scholarships

**TANGAZO** la maombi ya ufadhili wa masomo ya sayansi kupitia Samia Scholarship kwa mwaka wa masomo unaoanza Novemba mwaka huu limetolewa na wasomi wanaowania fursa hiyo kazi kwao kuomba.

Wasomi waliopata ufadhili mwaka jana walikuwa 636 na mwaka huu ni 640 idadi ambayo serikali inasema mfuko wa uhisani wa Samia uko tayari kuwafadhili kwa asilimia 100.

Ufadhili huo ulianza mwaka jana kwa wanafunzi 636 wakiwamo wasichana 261 na wavulana 375 na wenye mahitaji maalum walikuwa 12. Katika mwaka wa fedha 2023/24, wizara inatarajia kuchukua wanafunzi wengine 640 waliohitimu kidato cha sita na kwamba Shilingi bilioni 6.7 zimetengwa kugharamia wanafunzi wa zamani wanaoendelea na wapya wanaotarajiwa kuanza masomo.

Kikubwa ni vigezo, ili upate nafasi ni sharti mwanafunzi afikie ufaulu wa kiwango cha juu katika masomo ya sayansi na hisabati, vinginevyo ataondolewa kwenye ufadhili huo na hivyo kulazimika kurudi katika mfumo wa kuomba mikopo, ili aweze kuendelea na masomo ya juu.

Hayo ni kwa mujibu wa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, wakati akitangaza ufadhili huo kwa mwaka 2023/2024, wiki iliyopita na kufafanua kuwa serkikali imetenga bilioni 6.7.

Katika ufafanuzi wake, anasema fedha hizo ni kwa ajili ya ufadhili wa Samia scholarship na kwamba wanafunzi waliopata ufaulu wa juu katika masomo ya sayansi kwenye mitihani ya kidato cha sita, watanufaika.

Binafsi ninaona kwamba vigezo na masharti hayo, wanafunzi wasivichukulie kama kikwazo, bali vigeuzwe kuwa fursa ya kuwafanya wajitahidi katika masomo yao, ili waendelee kupata ufadhili huo.

Ufadhili huo unahusisha ada ya mafunzo, posho ya chakula na malazi, posho ya vitabu, mahitaji maalum ya vitivo, vifaa saidizi kwa wenye mahitaji maalum na bima ya afya.

Hivyo, ninadhani ni vyema kila mwanafunzi afikie viwango hivyo vilivyopendekezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ili nchi iandae wataalamu wengi zaidi wa fani mbalimbali wa baadaye.

Lakini vigezo na masharti hayo visichukuliwe kama njia ya kuwakomoa wanafunzi, bali viwafanye wawe na bidii, ili hatimaye wapate matokeo mazuri na kulipiwa ada katika masomo ya elimu ya juu.

Ninaamini kuwa wangu, serikali imedhamiria kupata wataalamu wengi wa fani mbalimbali wa baadaye, hivyo suala na kuweka vigezo na masharti ni kutaka lengo lifikiwe kwa viwango vya ufaulu vinavyotakiwa.

Hivyo, niwatie moyo wanafunzi kwamba wasikate tamaa badala yake wapambane ili wafikie viwango vilivyowekwa wizara kwa manufaa yao ili wasaidiwe katika mikopo kwa masomo ya juu.

Vilevile, ingizo jipya la wanafunzi, ambalo sasa zinawafanya wanufaika wote kufikia 1,276 kwa mwaka huu wa 2023, iwe ni hatua ya kuwahamasisha wanafunzi wa kidato cha sita kupambana hadi wafaulu kwa viwango.

Tayari serikali imeshaweka vigezo na masharti, hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi wa masomo hayo kufanya kila liwezekanalo kuhakikisha anafanya vizuri katika masomo hayo.

Jambo la msingi la kutambua ni kwamba, masomo hayo ndio yanatoa wataalamu wa fani mbalimbali, na ninaamini serikali inayakazania hadi kuweka uafadhili wa Samia Scholarship kwa sababu hiyo.

Lakini pia kwa mujibu wa Profesa Mkenda, nchi nyingi duniani zinazoendelea ni zile ambazo zinategemea ubunifu zaidi katika utafutaji maendeleo ya wananchi wake kwa kuwa ubunifu ni nguzo kubwa.

Maana yake ni kwamba elimu ni namba moja kwa nchi nyingi duniani kwa kuwa kupitia elimu inapatikana teknolojia na ubunifu, hasa kwa kusoma masomo ya sayansi ambayo ndio msingi wa ubunifu.

Ninaamini ufadhili wa Samia Scholarship unalenga kupata wataalamu wengi zaidi na wabunifu wa teknolojia mbalimbali watakaosaidia kuleta maendeleo katika taifa lao, hasa kwa kuzingatia vigezo na masharti.

## HABARI KITAIFA

### Polisi: Wanafunzi acheni tamaa ya vitu vidogo

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MKUU wa Dawati la Jinsia la Jeshi la Polisi mkoani Morogoro, amewataka wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kuacha tamaa ya vitu vidogo vidogo ambavyo huwapelekea mwisho mbaya ikiwamo kubakwa, kulawitiwa na mimba za utotoni.

Suleiman Kova alitoa angalizo hilo jana wakati wa mkutano wake na wanafunzi wa shule 10 za sekondari ulioandaliwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya Wezesha Mabadiliko (WEMA) ambayo pia imegawa taulo za kike za kufua 300 kwa wanafunzi hao.

Kova alisema Dawati la Jinsia la Jeshi la Polisi limekuwa linapokea wastani wa kesi nne hadi tano za mimba za utotoni kwa siku, sababu kubwa ikiwa ni tamaa ya kupenda 'lifti' na chipsi.

Alivitaja ni vitu vinavyosababishia madhara makubwa kwa wanafunzi kwa kuwa wahusika huwatumia na kuwaacha au kuwakimbia hata kama wamewapa ujauzito.

"Ukimkamata hata huyo aliyempa mimba, anakataa lakini akibanwa, ndipo utakuja kugundua kuwa alikuwa na uhusiano naye na ndiye amempa mimba.

"Hivyo, muwe na tahadhari, hawakubali! Utateseka na kulea mwenyewe ujauzito huku umekatishwa malengo yako," alionya.

Akitoa mada ya hedhi salama, Ofisa Ustawi wa Jamii wa Mahakama za Watoto, Anjela Banzi, aliwashauri watoto kujenga tabia ya kutoa taarifa pale wanapofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wazazi au walezi wao, walimu, ustawi wa jamii, polisi kata na katika vituo vyovyote vya polisi vilivyo karibu nao hata kama wanatishiwa kuuawa na waliowatenda kwa kuwa hakuna mtu mwenye mamlaka ya kumuua mwenziwe.

Aliwataka wanafunzi kuzingatia na kuitumia elimu ya hedhi salama wanayopewa kwa kuwa kama wasipokuwa salama, wana uwezekano wa kupata magonjwa ikiwamo fangasi na pengine kuwa wagumba baadaye, kuwa na msongo wa mawazo unaopelekea ugonjwa wa afya ya akili.

Akisoma taarifa ya kazi, Ofisa kutoka WEMA, Pia Schlitienbaver, alisema taasisi hiyo imeamua kugawa taulo hizo baada ya kufanya utafiti na kubaini kuwa mwaka 2021 wanafunzi 17 kati ya 100 hawakufika shuleni katika manispaa hiyo kutokana na changamoto za hedhi ikiwamo maumivu makali na kutokuwa na taulo za uhakika.

Alisema kuwa mwaka 2022 walifanikiwa kugawa taulo 250 na mwaka 2023 wamegawa 300 kwa wanafunzi wa shule 10 huku wakiwa na nia ya kugawa taulo 1,000 kwa kila mwaka. Wanawaomba wadau wa elimu kuwa na mwamko wa kuwasaidia wanafunzi pale inapobidi.

Mkurugenzi wa WEMA, Dk. Lusako Mwakiluma, aliwataka wanafunzi kuwa wanaposaidiwa nao wajisaidie kwa kuonyesha utulivu na bidii katika kukuza viwango vyao vya taaluma darasani.

Dk. Mwakiluma alisema taulo za kufua kwa wanafunzi ni nzuri kwa sababu zina uwezo wa kurudisha tabasamu lao huku zikitumika kwa mwaka mmoja na miezi minane na kuokoa kiasi kikubwa cha fedha kwa wazazi wao.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Jenga Afya Tokomeza Umaskini (JATU PLC), Peter Gasaya, akitoka Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana kusikiliza mashtaka yanayomkabili ya kujipatia Sh. bilioni 5.1 kwa njia ya udanganyifu. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Watu 12 wahofiwa kufa maji

## •TMA yatahadharisha

**Na Faustine Feliciane**

WATU 12 wanahofiwa kufa maji baada ya mitumbwi miwili kuzama Ziwa Victoria katika eneo la Mchigondo, Wilaya ya Bunda mkoani Mara.

Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Vicent Anney, alithibitisha kuwa chanzo ni hali mbaya ya hewa na kwamba watu 14 waliokolewa na kwa sasa wanaendelea kutafuta miili ya wengine 12 wanaodhaniwa kufa maji katika ajali hiyo.

Alisema mpaka jana jioni hakuna mtu aliyeokolewa wala mwili na juhudi za kusaka watu hao zinaendelea.

"Zoezi la uokoaji linakwamishwa kwa kiasi kikubwa na hali mbaya ya hewa, kuna upepo mkali sana unaosababisha mawimbi makubwa pamoja na kuongezeka kwa tope, lakini bado juhudi zinaendelea za kutafuta watu wengine 12," alisema Anney.

Aliwaomba wananchi kuchukua tahadhari kwa wakati huu kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa kwenye ziwa hilo.

Wakati huo huo, Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA), imeendelea kutoa tahadhari ya kuwapo kwa upepo mkali na mawimbi makubwa katika maeneo ya ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi, maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na TMA, unatarajiwa upepo unaofikia kilometa 40 kwa saa na mawimbi makubwa yanayofika mita mbili katika maeneo hayo ya mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Lindi, Mtwara na Zanzibar, Mwanza, Simiyu, Kagera, Geita, Mara, Kigoma, Katavi na Rukwa.

Akizungumza na gazeti hili, mtaalamu wa Hali ya Hewa wa TMA, Joyce Makwete, aliwataka wananchi katika maeneo hayo kuchukua tahadhari kukabiliana na hali hiyo.

"Hali hii tunaitarajia kutokea kuanzia Jumatano (kesho) mpaka Ijumaa na kwa mujibu wa mifumo ya hali ya hewa, uwezekano wa kutokea ni mkubwa," alisema Joyce na kuongezea;

"Athari zake ni pamoja na kukwama kwa shughuli za uvuvi na usafirishaji na shughuli nyingine za kiuchumi," alisema Joyce.

Aidha, alisema wananchi wasipuuze taarifa za tahadhari zinazoetolewa na mamlaka hiyo na wanapaswa kuchukua hatua kuepuka madhara na athari zinazoweza kutokea.

"TMA inaendelea kufuatilia mifumo ya hali ya hewa na tutaendelea kutoa taarifa kwa wananchi, tunaomba sana wananchi kufuatilia taarifa za hali ya hewa tunazozitoa kila wakati," alibainisha Makwete.

# Kinana aonya wananchi kuwaomba madiwani fedha

**Na Beatrice Shayo,** TABORA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kanali mstaafu Abdulrahman Kinana, amesema madiwani wanaponzwa na kujiita waheshimiwa, akiwataka wananchi waache mchezo wa kuwaomba fedha kwa kuwa hawana mshahara.

Kinana alitoa kauli hiyo jana katika mkutano wa wanachama wa CCM mkoani Tabora, akifafanua kuwa madiwani hawana mishahara, wanaishi kwa posho.

Alisema kinachowaponza ni kujiita waheshimiwa huku wananchi wakifika kwao kuwalilia shida zao wakati hawana mshahara.

"Madiwani wanalipwa posho tu, hawana mishahara kwa sababu wanaojiita waheshimiwa basi mtu, ana shida yake binafsi, anakwenda kwa diwani ampe fedha, anaugulia diwani ndio atoe fedha ya matibabu. Ana safari zake binafsi diwani ndiye atoe fedha. Akijibu hana fedha, nongwa inaanza tutakukata mwaka 2025," alisema Kinana.

Pia alisema wabunge wa Tanzania wanalipwa mshahara mdogo kuliko wabunge wote wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, akizitolea mfano nchi za Congo, Kenya, Uganda na Rwanda, alizodai mishahara ya wabunge wake iko juu.

"Hawa wabunge hata kuomba kuongezwa kidogo wanaogopa, tukisema tuwaongezee mtasikia kelele zake, tutafute namna ya kuwasemehe.

"Wabunge wakirudi jimboni kila mtu hodi, anataka apewe fedha, wakati mwingine mtu anafunga safari nauli hana, mbunge ndiye ampe. Akieleza hana 'tutakutana 2025 tunakutoa', si sawa hata kidogo," Kinana alionya.

Kinana pia alisema kama mbunge anafanya vizuri, anawaletea maendeleo, barabara, huduma za afya, shule na maji, hakuna haja ya kumtoa.

Alisema kubadilisha wabunge kama mashati, yaani kila mwaka wa uchaguzi, wanasababisha kukosa maendeleo, hivyo waache huo mchezo.

Kinana akitolea mfano Waziri Mkuu mstaafu, Cleopa Msuya, alipokuwa Mbunge wa Same, alipeleka maendeleo makubwa jimboni kwake na wananchi waliendelea kumwamini na kuendelea kuwaongoza kwa kipindi kirefu.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# CRDB yatangaza faida ya bilioni 260/- robo ya pili ya mwaka 2023

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imeendeleza ufanisi kwa kupata faida ya Sh. bilioni 265 kabla ya kodi katika miezi nusu ya kwanza ya mwaka sawa na ongezeko la asilimia sita kulinganishwa na Sh. bilioni 250 iliyopata kipindi kama hicho mwaka 2022.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema mwishoni mwa wiki iliyopita kuwa ongezeko la faida hiyo linadhihirisha utekelezaji makini wa mpango mkakati wake mpya wa miaka mitano kuanzia mwaka 2023 mpaka 2027 uliozinduliwa mapema mwaka huu.

Vilevile, Nsekela alisema faida iliyopatikana imechangiwa na uimara wa kiutendaji ingawa kumeshuhudiwa kuongezeka kwa gharama za uendeshaji. Uwekezaji uliofanywa wa kufungua tawi la Benki ya CRDB Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kuanzishwa kwa kampuni tanzu ya CRDB Insurance Limited kumeongeza gharama, lakini kutakuwa na matokeo chanya kwa siku zijazo.

"Faida tuliyoipata katika kipindi hicho imetokana na kukua kwa mapato yetu yaliyopanda kwa asilimia tisa kwa mwaka huo hasa yale ya riba yaliyoongezeka kwa asilimia 26 na kufika Sh. bilioni 192 kutoka Sh. bilioni 175 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Mapato yasiyo ya riba nayo yalikua kwa asilimia saba na kufika Sh. bilioni 106," alisema Nsekela.

Hata thamani ya mali za benki, mkurugenzi huyo alisema imeongezeka kwa asilimia 22 ikipanda kutoka Sh. trilioni 10.2 katika robo ya pili ya mwaka 2022 mpaka Sh. trilioni 12.5 mwaka huu.

Ongezeko hilo la thamani ya mali za benki, alisema Nsekela kuwa limechangiwa zaidi na kukua kwa mikopo iliyotolewa ambayo ndani ya mwaka mmoja uliopita imepanda kwa asilimia 29 kutoka Sh. trilioni 5.9 mpaka Sh. trilioni 7.6.

"Wakati kiasi cha mikopo tuliyoitoa kikipanda, uwiano wa mikopo isiyolipwa na jumla ya mikopo yote umezidi kushuka, ukipungua kutoka asilimia 2.8 mpaka asilimia 2.7. Hali hii inadhihirisha umakini wa benki yetu kudhibiti vihatarishi vilivyopo, hivyo kuifanya iendelee kuwa na wadaiwa wazuri wenye uhakika wa kulipa," alisisitiza Nsekela.

Hata amana, taarifa za benki hiyo zinaonesha zimeongezeka kwa asilimia 23 kutoka Sh. trilioni 7.1 mwaka 2022 mpaka Sh. trilioni 8.7 mwaka 2023, hivyo kuipa uwezo mkubwa zaidi wa kuwakopesha wateja wake wenye uhitaji nchi nzima kupitia mtandao wake mpana wa matawi 260 yaliyosambaa katika halmashauri zote.

"Katika robo hii, tumewakopesha sana wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kutambua mchango wao katika kukuza uchumi wa Taifa na kukuza ajira nchini.

"Ndani ya muda huo, tumeimarisha mtandao wetu wa matawi kwa kufungua mapya manne ili kusogeza huduma kwa wananchi. Tulizindua tawi letu wilayani Kaliua na Igunga mkoani Tabora halafu Bukombe kule Geita na Kilwa mkoani Lindi. Hizi zote ni juhudi za kuhakikisha tunakidhi matarajio ya wateja wetu kwa kuwafuata mahali popote walipo nchini," alisema Nsekela.

Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya CRDB, Fredrick Nshekanabo, alisema huduma za kidijiti zimechangia kwa kiasi kikubwa ufanisi wao kwa kuwa siyo tu unamruhusu mteja kukamilisha muamala muda wote bali pia unampa fursa hata akiwa nje ya mipaka ya Tanzania.

Katika robo ya pili mwaka huu, mkurugenzi huyo alisema Benki ya CRDB imezindua kampeni mbili ambazo ni Benki ni SimBanking na CRDB Wakala '10 na Kitu' ili kuhamasisha matumizi ya njia mbadala kupata huduma ambazo zinaendelea kutekelezwa.

Nshekanabo alisema zimedhihirisha kuwa muhimu sokoni kwa kuwa zimechangia ongezeko la majukwaa hayo. Kwa sasa asilimia 96 ya miamala yote ya benki hiyo inafanyika kidijiti.

"Programu mpya ya SimBanking ina vitu vingi vya ziada vinavyokidhi matarajio binafsi zikiwamo fursa za uwekezaji katika akaunti ya muda maalum. Kwa siku zijazo tunatarajia kuimarisha zaidi huduma za kidijiti. Ili kuimarisha faida yetu, tunayo mikakati ya kupunguza gharama za uendeshaji," alisema Nshekanabo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkenda asifu uhusiano Tanzania, Morocco

**Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema uhusiano kati yake na Morocco unaendelea kukua siku hadi siku, hususani ziara za kikazi kwa viongozi wa nchi hizo mbili, akiwamo Mfalme Mohamed VI kuzuru nchini.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda aliyasema hayo jijini Dar es Salaam katika hafla na ya kuadhimisha miaka 24 ya Mfalme Mohamed VI wa Morocco tangu atawazwe kushika kiti hicho.

Kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, ninatoa pongezi kwa Serikali na Ufalme wa Morocco wakati mkitimiza miaka 24 ya Mfalme Mohamed VI tangu alipotwaa kiti cha ufalme.

"Tunasherekea pamoja na Morocco katika maadhimisho haya. Na Morocco inabakia kuwa ni taifa lililojawa na utajiri wa kiutamaduni," alisema Prof. Mkenda aliyekuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo.

"Ziara ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Morocco mwaka 2021 na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson na Naibu Spika, Azan Zungu na ujio wa Mfalme Mohamed VI nchini mwaka 2016, ni ishara ya uhusiano mwema," aliongeza Prof. Mkenda.

Alisema Morocco imeendelea kutunza historia yake na utamaduni licha kuwapo mabadiliko ya dunia katika maendeleo ya kijamii yatokanayo na wakati.

Prof. Mkenda pia alisema nchi hizo mbili zimeendelea kutia saini makubaliano ya kushirikiana katika shughuli mbalimbali za maendeleo, ikiwamo biashara na miradi mingine ya kiuchumi.

"Tumeshuhudia uchumi kati yetu ukikua na Tanzania imekuwa inapeleka biashara Morocco inayokadiriwa kuwa Sh. bilioni 24.9. Bado tuna safari ndefu," alisema Prof. Mkenda.

Alieleza kwamba kutokana na jiografia ya nchi hizo mbili, kuna fursa ya uwekezaji kwa wawekezaji wa Tanzania na Morocco.

Kuhusu elimu, Prof. Mkenda alisema Tanzania inafurahia fursa za ruzuku ya elimu inayotolewa na Morocco, wanafunzi kwenda kusoma katika nchi hiyo katika fani tofauti.

Balozi wa Morocco nchini, Zakaria El Goumiri, alisema kuwa kutokana na uwajibikaji thabiti wa Mfalme Mohamed VI wa Morocco, kuna matokeo chanya ndani ya nchi hiyo na barani Afrika.

"Tangu Mfalme Mohamed VI wa Morocco aweke jitihada katika ukuzaji uchumi katika sekta za kilimo, utalii na nishati, kumekuwa na fursa nyingi za kiuchumi.

"Kuna program maalumu za kuhakikisha kunafikiwa maendeleo katika jamii kama vile afya, elimu kwa maeneo yote mijini na vijijini, haki na usawa," alisema.

Balozi huyo pia alisema nchi ya Morocco imejikita katika kuhakikisha kunafikiwa usawa wa kijinsia, hususani katika nyanja ya kisiasa kwa kuhakikisha kuna uwakilishi ulio sawa.

Balozi Zakaria alisema Morocco pia imeweka kipaumbele katika kutunza kumbukumbu na makumbusho na imetoa ruzuku ya masomo kwa wanafunzi takribani 20,000 kusoma Morocco.

"Mwaka huu tunalenga kuwafikia wakulima 40,000 katika mikao ya Mara, Geita, Tabora na Kagera katika miradi ya kupima udongo na kuwafunza. Tutaendelea kushirikiana," aliahidi Balozi huyo.

# Pinda ahimiza uadilifu kwa viongozi serikalini

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amesema viongozi wa serikali wanatakiwa kuwa waadilifu na wenye hofu ya Mungu katika utendaji wao wa kazi na kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Pia amesema ni muhimu viongozi wa ndani ya serikali kuwajibika kikamilifu na kutanguliza uzalendo kwanza ndipo wadai haki yao.

Alitoa kauli hiyo jana alipofungua mafunzo ya uongozi kwa viongozi wa taasisi na mashirika ya umma katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere iliyopo Kwamfipa, wilayani Kibaha, mkoani Pwani.

Alisema yapo mashirika na hata idara za serikali ambazo zinayumba kwa sababu ya baadhi ya watu kukosa uadilifu katika utendaji kazi wao, jambo linalopaswa kukomeshwa.

"Kuweni na uadilifu na hofu ya Mungu katika utendaji wenu. Kwa kufanya hivi itawafanya kuacha maovu ambayo yanaathiri jamii mnayoitumikia," alionya.

Pinda pia alisema vyuo kama cha Mwalimu Nyerere vitasaidia kujenga uwezo wa makatazo sehemu za kazi, pia semina za mara kwa mara kwa viongozi kuhusu mambo ambayo yanatakiwa kuwa endelevu ni muhimu.

"Kozi fupifupi hata walioko serikalini kutoa elimu katika maeneo ambayo yana makatazo ni muhimu. Ipo haja kuwa na utaratibu huu ili kuwaweka katika malengo sawa na wanaonufaika hapa wakitoka wakaelimishe wale waliobaki ili kwenda sawa," alisema.

Mkuu wa Shule hiyo ya Uongozi, Prof. Macellina Chijoriga, alisema yako baadhi ya mashirika yamekuwa hayafanyi vizuri kama ilivyotarajiwa, hivyo mafunzo kama hayo yatasaidia kuondoa vikwazo.

Alisema viongozi wanatakiwa kuwa waadilifu, waaminifu na wabunifu na kwa kupitia mafunzo hayo ya siku sita, mategemeo ni kuona matokeo chanya kwa washiriki na taasisi walizotoka.

Alisema washiriki wa mafunzo katika chuo hicho wamekuwa wanafundishwa masomo mbalimbali ikiwamo historia ya vyama sita vya ukombozi na utawala bora.

Alisema kozi hiyo ni ya 19 tangu kuanzishwa kwa shule hiyo na tayari wahitimu 219 wamepata mafunzo na taasisi zaidi ya 40 zimeitumia shule hiyo kupeleka wawakilishi wake kunufaika na mafunzo.



## Zaidi ya watoto 200,000 wapatiwa chanjo surua, polio

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WATOTO 227,072 wenye umri chini ya miaka mitano mkoani Manyara, wamepatiwa chanjo ya surua na polio kwa mwaka 2022 kwa ajili ya kuwakinga wasiambukizwe maradhi yanayotokana na surua na virusi vya polio.

Aliyasema hayo jana Mratibu wa Chanjo mkoani Manyara, Sulaiman Manoza, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu hali ya utoaji wa chanjo hiyo kwa watoto.

Manoza, alisema kwa chanjo ya surua mkoani humo, ililenga kuwachanja watoto 75,263, lakini tayari wamewachanja watoto 78,507 kwa dozi ya kwanza sawa na asilimia 104.

Alisema dozi ya pili ya chanjo ya surua walichanjwa watoto 70,876 sawa na asilimia 94 ya watoto waliolengwa.

Pia, alisema kwa chanjo ya polio walilenga kuwachanja watoto 75,263 ambao walikuwa chini ya mwaka mmoja na wamefanikiwa kuwachanja watoto 77,689 sawa na asilimia 103.

Mtaalamu huyo alieleza kuwa chanjo zote wanalenga kuwachanja watoto chini ya miaka mitano.

Naye Meneja wa Mpango wa Chanjo Taifa, Dk. Florian Tinuga, akizungumza na waandishi wa habari wa Kanda ya Kaskazini jijini hapa, alisema suala la upatikanaji wa chanjo siyo tatizo bali shida iko kwa wazazi kuwapeleka watoto.

Dk. Tinuga, alisema kati ya mwaka 2019 hadi 2022 liliachwa kundi la watoto chini ya miaka mitano wengi hawakukamilisha dozi kwa kuwa wazazi wao hawakuwapeleka.

Mkazi wa Kijiji cha Gallapo, Amina Musa, alisema suala la chanjo kwa wazazi wengi wanatambua na kuiomba serikali isogeze huduma maeneo ya vijiji ambayo hayana zahanati.

Mkazi wa Mtaa wa Negamsi,John Martine,alisema chanjo inaimarisha kinga ya mwili na kuzuia magonjwa ndio maana wazazi hawaipuuzi kwa watoto wao.

# Tanzania, Ghana kuonesha bidhaa wanazozalisha

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA na wajasiriamali kutoka Ghana na Tanzania wanatarajia kujumuika pamoja na kuonyesha bidhaa wanazozalisha ili kuinua uchumi wa nchi zao na vipato vyao.

Maonesho hayo yataanza Septemba 25 hadi 29 mwaka huu, jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wajasiriamali 70 kutoka Ghana na 50 kutoka Tanzania.

Akizungumza jana jijini Arusha na waandishi wa habari kuhusu onesho hilo lililopewa jina la Ghana Expro 2023 Tanzania, Balozi wa Ghana kwa nchi za Afrika Mashariki, Damptey Bediako, alisema onesho hilo ni sehemu ya Ghana kuimarisha uhusiano wa kiuchumi na Tanzania.

Alisema Ghana imekuwa na uhusiano mzuri na Tanzania tangu utawala wa marais Hayati Julius Nyerere na Dk. Kwame Nkrumah waliokuwa wakishirikiana katika harakati za kupigania uhuru wa Afrika.

"Wakati viongozi hawa wawili wakiongoza harakati za kupigania uhuru wa kisiasa ni imani yetu kuwa onyesho hili litakuza undugu wa mataifa haya," alisema Bediako.

Alisema siku tano zitahusisha maonesho ya bidhaa, semina, mijadala ya watu mashuhuri kutoka Ghana na Tanzania itakayohusu maendeleo ya kiuchumi na kuimarisha uhusiano.

Aliwakaribisha Watanzania na raia wa Ghana wanaoishi Tanzania kuja kushiriki maonesho hayo ambayo yataambatana na matukio mbalimbali.

Mkurugenzi wa Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), Mwajuma Hamza, alisema jukumu lao ni kuhakikisha wanawake wajasiriamali wananufaika na Jukwaa Huru la Afrika.

Alisema katika onesho hilo, TWCC inatarajia kutangaza bidhaa zinazozalishwa hapa nchini korosho, asali, kahawa ambazo zitapewa kipaumbele.

Hata hivyo, aliwakaribisha wanawake wajasiriamali kushiriki katika onesho hilo ili kuangalia fursa zilizopo na kuuza bidhaa zao katika masoko ya kimataifa.



Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Msingi wa TAMISEMI, Suzani Nusu (wa pili kulia), akikagua ujenzi wa mabweni na madarasa katika Shule ya Sekondari ya Muheza juzi kwenye Kijiji cha Mwembeni, Kata ya Magoroto. Miradi hiyo inajengwa kwa fedha za Boast. **PICHA:STEVEN WILLIAM**

# Ndalichako awaonya wafanyakazi hoteli lugha mbaya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Profesa Joyce Ndalichako, amewakemea baadhi ya wafanyakazi wa hoteli wanaotoa lugha mbaya na kutumia simu za mkononi, wakati wakiwahudumia watalii.

Akizungumza jana jijini hapa wakati akifunga mafunzo ya kukuza ujuzi kwa wafanyakazi wa hoteli, yaliyoratibiwa na wizara hiyo, kuboresha huduma za hoteli kwa watalii, Prof. Ndalichako, alisema anaamini mafunzo hayo yatawezesha watalii kupata huduma bora watakapotembelea vivutio vilivyoko nchini.

"Tumetoa mafunzo haya kwa kuanza na Arusha, kwa sababu baada ya utafiti tuliofanya katika hoteli 35 tulibainia utoaji wa huduma zisizoridhisha kwa wateja, lugha mbaya, matumizi ya simu ya kiganjani wakati mteja anasubiri huduma na ukosefu wa ujuzi wa kihudumia wateja," alisema.

Alisema Rais Dk. Samia Hassan Suluhu anahitaji kuona wafanyakazi wa hoteli wanakua na ujuzi wa kutoa huduma bora ili kuvutia watalii kutamani kurejea Tanzania wanaporejea kwao.

"Kila mmoja wenu katika nyanja hii mjitafakari katika utoaji wa huduma kwa wageni wetu, maana wengine unakuta mteja anaagiza mboga za majani aina hii unaleta nyingine, lakini chakula chenyewe mafuta yamejaa wakati wengi siku hizi hawahitaji mafuta hasa nyakati hizi za ongezeko la magonjwa matokeo yake mgeni anaaga na kuhamia hoteli ya jirani yako," alisema.

Kadhalika, alisema serikali imeanzisha programu hiyo, kusaidia kukuza ujuzi kwa wafanyakazi wa hoteli ambao wengi ni vijana na wameingia katika ajira bila kuwa na ujuzi stahiki.

"Hatuwezi kuwaacha kuendelea kufanya kazi hii, bila ujuzi na ndio maana tumeamua kutengeneza mifumo ya kukuza ujuzi kwenu, ili mtoe huduma stahiki kwa wageni wetu," alisema.

Aidha, alisema serikali baada ya kutoa mafunzo hayo, watafuatilia kuona mafanikio yake na kuboresha pale panapohitajika.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Jamal Katundu, alisema programu ya kukuza ujuzi kwa wafanyakazi wa hoteli imeanzia Arusha kwa kuwa ni kitovu cha utalii.

"Tulibaini katika utafiti wetu wageni wengi hasa wa naotoka nje ya nchi hawapendi kufikia hoteli za kati sababu ya huduma zinazotolewa huko siyo stahiki, kutokana na hilo imesababisha tutoe mafunzo kwa ajili ya kuboresha huduma zao kwa lengo la kuongeza wageni," alisema.


Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Henry Mkunda, aliwataka wafanyakazi waliopata mafunzo hayo kubadilika na kuvutia wageni wengi zaidi kuja nchini.

"Tunapotoa huduma bora watalii watarudi tena nchini na tulinde heshima tuliyonayo kwa kuwa kwa sasa Tanzania ni ya pili Afrika kupokea wageni wengi zaidi hivyo pamoja na jugudi za Rais Samia za kuvutia watalii alinazofanya na sisi tunahitaji kuboresha huduma zetu ziwe bora zaidi ya huko nyuma tulizokua yunatoa," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Raphael Maganga, aliomba serikali iendelee kushirikiana na seka binafsi kuboresha zaidi huduma za watalii nchini.

"Lakini tunaomba serikali itusaidie na sisi wa hoteli za kati tupate wageni hasa hawa weupe wa nje ya nchi, kwa kuwa wakija hawafiki kwetu hivyo na sisi tunahitaji kuwapokea na kuwahudumia,lakini tumeboresha sera za wafanyakazi na waajiri ili pande zote zinufaike bila kuumiza upande mwingine," alisema.

Mwakilishi wa hoteli daraja la kati, Alex Mariwa, aliomba serikali itengeneze utaratibu wa kuwezesha hoteli za kati kupokea watalii wa nje ili wanufaike hasa nyakati hizi za mafuriko ya watalii baada ya filamu ya The Royal Tour.





# Wahandisi watakiwa uwajibikaji kwenye miradi ya maendeleo

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

KIONGOZI wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, Abdallah Shaib Kaim, amewataka wahandisi wa halmashauri nchini kusimamia kwa umakini miradi ya maendeleo inayogusa maisha ya wananchi, ili iwe yenye kiwango cha juu na kukidhi thamani ya fedha.

Alitoa agizo hilo juzi wilayani Kishapu wakati akikagua na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo ya sekta ya elimu, maji, afya, miundombinu ya barabara na mazingira.

Alisema katika baadhi ya miradi waliyotembelea ikiwamo Kituo cha Afya Negezi, wilayani Kishapu, ujenzi wake ni mzuri lakini umaliziaji wake ni wa kiwango cha chini huku akiwataka wahandisi kufanyakazi kwa umakini mkubwa.

"Wahandisi wa halmashauri kazi yenu ni kuisaidia serikali kusimamia miradi ya maendeleo ambayo imekuwa ikitekelezwa na kutoa ushauri kwa makandarasi au mafundi, baadhi ya miradi niliyopitia upungufu kidogo sana sababu ya nyie kushindwa kuisimamia vizuri," alisema Kaim.

Aidha, aliagiza pia mifuko 11 ya saruji ambayo haionekani kwenye nyaraka katika ujenzi wa Kituo cha Afya Negezi wilayani humo, irudishwe haraka kabla ya siku tano na apewe taarifa ili kuzuia ubadhilifu kwenye utekelezaji wa miradi.

Katika hatua nyingine akizindua Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria Kijiji cha Masagala, alizindua gari la wagonjwa lililonunuliwa na wachimbaji wadogo wa dhahabu Mwakitolyo namba tano wilayani Shinyanga kwa ajili ya Zahanati ya Mwakitolyo.

Aidha, aliwataka wakazi wanaofikiwa na mradi huo wa maji kutunza miundombinu ili kuepuka kukumbwa na adha ya upatikanaji wa maji huku akiwapongeza wachimbaji hao kwa kushiriki vyema katika kuboresha huduma za afya.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi, alisema gari la wagonjwa limekuwa msaada mkubwa katika utoaji wa huduma za matibabu kwa wananchi wa Mwakitolyo na vijiji jirani.

Baadhi ya wananchi wilayani Kishapu, Ester Gonji, waliishukuru serikali kwa utekelezaji mirdai mingi ya maendeleo ikiwamo ya afya, maji ambayo ni muhimu katika maisha ya kila siku.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa akimsikiliza mkandarasi wa kampuni ya Synohydro Corporation Limited inayojenga barabara ya Kanyani Junction hadi Mvungwe yenye urefu wa Kilomita 70.5 mkoani Kigoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madiwani wazipa 'tano' shule mbili zilizofaulisha

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

BARAZA la Madiwani wa Manispaa ya Kahama, wameupongeza uongozi na wanafunzi wa shule mbili za kidato cha tano kwa kufanikisha ufaulu mzuri kwa mtihani wa kidato cha sita na kutokuwa na daraja la nne na sifuri.

Shule hizo ni Mwendakulima na Abdulrahim na kwamba zimeipa heshima manispaa hiyo huku wakitaka bidii hiyo kuendeleza kiwango cha ufaulu kinaongezeka.

Diwani wa Viti Maalumu wa Kata ya Nyasubi, Herita Makaga, akichangia hoja katika kikao cha robo ya nne cha Baraza la Madiwani wa Manispaa ya Kahama, alisema shule hizo zinapaswa kupongezwa na kuongezewa nguvu ili ufaulu wake uzidi kupanda.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, alisema kuna mpango wa kuendelea kuboresha huduma katika shule, ikiwa ni pamoja na kuongeza watumishi sekta ya elimu ili kuendelea kuongeza viwango vya ufaulu.

Kadhalika, alisema kuna shule mpya zinajengwa, vyumba vya madarasa vinajengwa sambamba na shule shikizi huku kukiwa na nyumba za walimu na kwamba kwa jitihada hizo lazima ufaulu utaongezeka.

**Shule hizo ni Mwendakulima na Abdulrahim na kwamba zimeipa heshima manispaa hiyo huku wakitaka bidii hiyo kuendeleza kiwango cha ufaulu kinaongezeka.**

# Madiwani wapewa jukumu marejesho mikopo wajasiriamali

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, Hamisi Katimba, amewataka madiwani kufuatilia kwa karibu vikundi vya ujasiriamali vilivyokopesha fedha za miradi mbalimbali zirudi kwa ajili ya kusaidia wengine.

Mikopo hiyo ni fedha zinazotokana na asilimia 10 ya mapato ya halmashauri ambayo hupewa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa muundo wa 4, 4, 2 ikiwa haina riba.

Katimba alitoa kauli hiyo juzi katika kikao cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2022/2023 cha Baraza la Madiwani cha Halmashauri, kwamba ni lazima fedha hizo zikarejeshwa ili zisaidie wengine.

Alisema kuwa wakati wa mchakato wa kuvikopesha vikundi hivyo, madiwani walikuwa mstari wa mbele kuvisimamia ili vipate mikopo hiyo, lakini kwenye kurejesha wanakaa kando jambo ambalo siyo sawa kwa kuwa wanapaswa kutumia nguvu ile ile kuhakikisha vikundi vinarejesha fedha za umma.

"Suala hili sio siasa kwa hiyo tusaidiane kuzirejesha kama mlivyokuwa mkivisaidia kukopa na ufuatiliaji huu tutaufanya kwa kushirikiana na ofisi yangu," alibainisha Katimba.

Diwani wa Ikinda, Matrida Musoma, alisema agizo hilo watalitekeleza kwa wakati kwa kuwa wanavifahamu vikundi hivyo na baadhi vinaendelea na shughuli zake kama kawaida.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Mibako Mabubu, alisema fedha hizo zinazotokana na asilimia 10 za mapato ya ndani ya halmashauri na kwamba lazima zirejeshwe na kuwataka madiwani kusimamia jambo hilo kwa ufasaha.

Wakati huo huo, Diwani wa Kinamapula, Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, Sharifu Samweli, alionesha kusikitishwa na vitendo vinavyofanywa na baadhi ya maofisa ugani wa kata kwa kutumia pikipiki walizopewa na serikali katika matumizi yao binafsi kama kuteka maji, badala ya kutoa huduma stahiki kwa wakulima juu ya kuboresha kilimo kuwa cha kisasa.

Alibainisha katika kikao kazi cha kuweka mikakati ya uendelevu wa mradi wa ufuatiliaji wa matumizi rasilimali za umma zilizotolewa kwa ajili ya kuboreshaji wa huduma za kilimo (PETS) unatekelezwa na chama wasioona Mkoa wa Shinyanga kwa ufadhili wa The Foundation for Civil Society.

"Maofisa ugani wote wanaotumia pikipiki hizi katika matumizi tofauti na yale yaliyolengwa na serikali, wawajibishwe kisheria kwa sababu wanakuwa wanahujumu serikali, tusipolikemea hili uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara hautaongezeka," alisisitiza Samweli.

Alisema, anashangaa kuona kila mwezi maofisa ugani hao wanaandika ripoti ya ukelezaji wao wa majukumu na kuiwasilisha katika halmashauri na huku hakuna kikao wala mikutano ya wakulima wanayoifanya na kuishauri serikali kufanya ufuatiliaji na pale watakapowabaini wawachukulie hatua za kisheria.

Ofisa upelelezi kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU) wilayani humo, Amos Mtaleni, alishangaa kuona yanapatikana mafuta ya kufanya shughuli binafsi, lakini ya kuwafikia wakulima na kuwapa elimu yanakosekana huku akiahidi kufuatilia kwa kina.



Ukurasa 12

Shule zinapoona ahueni pale zuio la bweni linapolegezwa



Ukurasa 13

Jihadhari usiwe kati ya 158,000 wanaokufa kila mwaka na dawa

Nipashe

# TESA

Jumanne Agosti 1, 2023

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




Ukurasa 14

**Wafugaji hapa ndipo ilipo nyama bora, ukuaji kasi mifugo na gharama nafuu**

SAYANSI

NA CHRISTINA MWAKANGALE

# Ndivyo nyuki alivyo mali kila kitu chake ni cha bei, thamani kubwa

- Anayo tiba ya uzee, anaumaliza ugumba sumu yake ghali hukaribia nusu milioni

MWAMBOGELA Gabriel, ni mwanasayansi, msomi anayetoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), ambaye amejikita katika kuyaendeleza mazao ya nyuki, kwa kuzalisha bidhaa mbalimbali na kuziingiza sokoni, ikiwamo asali, chavua, sumu, maziwa, jeli na mafuta.

Unaweza kujiuliza sumu ya nyuki ikoje? Gabriel anajibu kuwa ni iliyosababisha upate maumivu makali. Kuvimba na wakati mwingine hata kifo. Anajiita mwanasayansi wa nyuki na teknolojia yake, lakini ni mwatamizi na mhitimu wa Shahada ya Sayansi na Teknolojia ya Ufugaji Nyuki.

Anazungumza na Nipashe kwenye Banda la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), wakati wa Maonesho ya Sabasaba, akibainisha namna alivyojiajiri huku akizalisha bidhaa nyingi zinazomwingizia kipato.

"Ni mwanasayansi wa nyuki na teknolojia yake imebuni utaalamu wa kuvuna mazao yake. Kwanza inavyofahamika tunapozungumzia nyuki watu wengi wanawafahamu katika kutengeneza asali pekee lakini kuna zaidi ya hilo ni zao moja."

"Kitaalamu nyuki anatengeneza mazao sita, tunazungumzia wanaofugwa kwa sababu kwenye taaluma hii tuna aina 20,000 za wadudu hao, lakini katika aina hizo tunapata tatu ambazo mara nyingi wanafugwa," anabainisha msomi huyo.

Anasema katika ukanda wa Afrika, hususan Tanzania kuna aina kuu mbili za nyuki wanaofugwa, ambazo ni wanaodunga wakijulikana kisayansi kama nyuki wakubwa na aina ya pili ni wale ambao hawadungi wasio na mwiba, hao huitwa nyuki wadogo.



Mwambogela Gabriel, akiainisha bidhaa mbalimbali za nyuki anazosema zina thamani na umuhimu mkubwa kwa afya. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

Tukumbuke kuwa kiumbe kinachouma kina meno lakini nyuki hawana meno badala yake wana mwiba hivyo hudunga na kuacha 'kisindano' hicho kwa aliyeumizwa.

"Kitanzania tumewatenga kama nyuki wadogo na wakubwa, lakini kuna aina nyingine ya nyuki ambao wanapatikana ukanda wa Mediterranean wapo pia mataifa ya Afrika Kaskazini hawa wanasifika kwa kuzalisha chavua nyingi," anaeleza.

Gabriel anasema ameamua kufuga akisaka faida, ikiwamo kupata asali, gundi, mafuta, lishe na tiba ambayo humuongezea binadamu kinga na homoni na kuimarisha uzazi akiongeza:

"Tunafuga nyuki kwa ajili ya kupata mazao yake kama asali na pia nta tukija kwa huyo anayedunga, au nyuki mkubwa anazalisha chavua, nta, asali, sumu ya nyuki ambayo mtu akidungwa anavimba hii ni bidhaa. Pia anatupatia maziwa ya nyuki na gundi ya vyote vina thamani na huhitajika sokoni."

Akizungumzia maziwa anasema nyuki wana tezi maalumu la kuzalisha maziwa ambayo ni chakula cha malkia na nyuki wachanga.

Anakumbusha kuwa malkia hula maziwa maisha yake yote na kwamba wanamtengenezea chakula hicho mahusi na wafugaji wanapotaka kuyazalisha wanatengeneza seli za maliki ambazo zitawavuta kuongeza uzalishaji, kazi inayofanywa kitaalamu.

Gabriel anaongeza kuwa maziwa yake yanachanganywa kwenye asali na yana virutubisho vinavyozuia kuzeeka, huongeza kinga ya mwili na anayaelezea kuwa ni mazito yako kama 'cream'.

"Mazao ambayo nyuki anazalisha yote yana faida kubwa katika lishe, lakini kwenye tiba tukianza katika lishe kuna mazao kama asali, watu wengi wanatumia kama chakula ukiila unapata faida za kilishe, lakini faida za kiafya," Gabriel anaeleza.

Anatolea mfano kwa asali inayozalishwa na nyuki wadogo, ikitumiwa humwongezea mtumiaji virutubisho kwa kuwa wana sifa ya kipekee wakati wa kutengeneza asali hiyo na kuongeza:

"Asali ya nyuki wadogo, inasifika sana kitiba kutokana na aina ya virutubisho au vitu ambavyo vimesheheni. Wanaoitengeneza ni wale wasiodunga ambao kiumbo ni wadogo ndiyo maana wanapewa jina la nyuki wadogo."

Anawasifia kuwa wana uwezo wa kupenya katika maua ambayo ni madogo sana yanayowashinda wakubwa hawawezi kupita, hivyo wanakuwa na wigo mpana wa kutembelea mimea na maua tofauti tofauti na kukusanya maji maji ua malighafi zinazokuwa na faida kubwa kitiba. Asali hii ina kiwango kikubwa cha 'biotic compound' ambazo zinasaidia katika mfumo wa chakula lakini imesheheni utajiri."

Anafafanua kuwa 'biotic compounds' ni vitu vilivyo hai katika mimea na viumbe hai ambavyo vina sifa ya kutibu na kusema asali ya nyuki wadogo inasaidia umeng'enyaji wa chakula na sukari inayopatikana ndani yake ina utajiri wa sukari ambayo haipatikani sana katika nyuki wakubwa na kwamba husaidia kudhibiti ongezeko la kiwango kikubwa cha sukari kwenye mwili wa binadamu.

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA HALFANI CHUSI

# Shule binafsi zinapoona ahueni pale zuio la bweni linapolegezwa

MWANZONI mwa Machi mwaka huu, Wizara ya Elimu inapiga marufuku shule kulaza wanafunzi bweni kwa watoto wanaosoma masomo ya awali, darasa la kwanza hadi la nne isipokuwa kwa kibali cha Kamishna wa Elimu baada ya kupokea maombi na kuyachuja.

Hadi sasa ni miezi mitano tangu kutangazwa utaratibu huo ambao ulikomesha watoto kuishi mabwenini ifikapo Juni mwaka huu.

Ni tangazo la kuwanusuru wanafunzi dhidi ya vitendo vya ukatili uliokuwa umeshamiri ikiwamo ubakaji, ulawiti na hata kufanyiwa vitendo vingine visivyo vya kiungwana wanapokuwa mabwenini.

Hata hivyo, wamiliki wa shule za bweni wakiwamo wa shule binafsi wanafika kwenye milango ya Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Adolf Mkenda, kuangalia namna ya kuboresha agizo hilo, wakiwa na mada mkononi kwamba kuna watoto wengine usalama wao ni pale wanaposoma shule ya bweni na si kwingineko.

Akizungumza na Nipashe kuhusu uamuzi wa serikali kukubali kukaa na wamiliki wa shule, na kusikiliza maoni yao kuhusu zuio la bweni kwa wanafunzi wadogo Mwenyekiti wa Taifa Chama cha Wamiliki na Mameneja wa Shule Binafsi na Vyuo (TAMONGSCO), Alfred Luvanda, anashukuru serikali kusikia kilio chao.

Anasema uamuzi wa awali huenda ungeziua shule binafsi na kwamba hatua ya Waziri wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda, kukubali kukaa pamoja na viongozi wa shule binafsi kufanya malekebisho kwenye tamko la kuzuia watoto wadogo kusoma bweni imerejesha ahuweni na ari ya kufanya kazi kwa shule binafsi.

Anakumbusha kuwa tamko la waziri lililowataka kufunga shule za bweni, kuanzia darasa la kwanza hadi la nne liliibua sintofahamu kwa wazazi na walezi pamoja na wamiliki wa shule binafsi hasa za bweni kwa kuwa lilikuwa linaathiri moja kwa moja ustawi wao.



Wanafunzi wakifurahia maisha bwenini. **PICHA: MTANDAO**

> ...Sasa ni wakati wa kutambua mchango mkubwa unaofanywa na shule binafsi katika kuinua elimu nchini.

"Ninaweza kutoa mfano kidogo, unakuta askari ana mtoto anasoma na kituo chake cha kazi labda ni Sudani yupo Darfur, hakuna namna yule mtoto atapata malezi mazuri zaidi ya shuleni, kwa sababu nyumbani uangalizi wake unakuwa mdogo.

"Mwanadada amepata ujauzito, anafanya kazi Kariakoo na makazi yake yapo Mbagala na mtoto unakupata pengine amesusiwa amtunze peke yake, eneo sahihi kwa yule mtoto kupata malezi ni shuleni".

Anaongeza kuwa kwa sasa, wamepewa muongozo na serikali ambao upo vizuri kwa sababu, unaruhusu watoto wanaotoka kwenye mazingira hatarishi wabaki bweni, jambo alilosema kwa sasa wizara imejua kuwa vipo vikwazo hatarishi kwa watoto wote kuzuiliwa kusoma bweni.

Ni hoja inayoungwa mkono na kiongozi Mwandamizi wa Serikali ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ana Tibaijuka, akisema sasa ni wakati wa kutambua mchango mkubwa unaofanywa na shule binafsi katika kuinua elimu nchini.

Kadhalika anashauri shule binafsi, ziwekeze zaidi kwenye utoaji wa elimu ya sayansi kwa vitendo ili kuandaa kizazi kinachokwenda na wakati, kwa sababu tupo kwenye miaka ya kidigitali.

"Serikali tunaangalia namna ya kuziwezesha shule binafsi kupata mikopo nafuu, ili ziwekeze katika maabara na elimu ya vitendo, ili tupate wanafunzi wanaoweza kujitegemea hata bila ajira za serikali au sekta binafsi," anashauri.

### YA WALEZI, WAZAZI

Msafiri Iginas, mzazi wa mwanafunzi wa darasa la nne anasema wakati serikali imetangaza kuzuia wanafunzi kukaa bweni alisumbuka kupata namna ya kumsomesha mtoto wake kwa kuwa ni dereva wa malori.

"Mimi ni dereva sikai kabisa nyumbani kwa hiyo kama mwanangu hatasoma shule ya bweni, maana yake niache kazi niwe namlea kwa kumpeleka shule na kurudi jambo hilo lingenisumbua sana."

Mzazi mwingine Mariamu Salehe anasema uamuzi ungebaki vilevile ungemuathiri kwa sababu sio kila mzazi au mlezi ana nafasi ya kukaa na mtoto wake kama ilivyo kwa wengine.

Machi 6 mwaka huu, Kamishina wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa, anapiga marufuku watoto wadogo kukaa bweni. Kwa upande mwingine, Waziri wa Elimu Mkenda anakumbusha kuwa lilikataza kuwalaza mabwenini wanafunzi wa elimu ya awali na darasa la kwanza isipokuwa kwa kibali maalum kitakachotolewa na kamishna baada ya kupokea maombi kutoka shule inayotaka kuwaweka watoto hao bweni.

Kamishna Mtahabwa akitangaza anaongeza kuwa hatua hiyo ni utekelezaji wa mwongozo wa uanzishaji wa usajili wa shule uliotolewa na wizara Novemba 2020.

## Ndivyo nyuki alivyo mali kila kitu chake ni cha bei, thamani kubwa

**INATOKA UK.11**

Kadhalika, Gabriel anasema, kwa watu wenye kisukari wanashauriwa kutumia asali ya nyuki wadogo, kwa sababu aina zake za sukari hazisababishi kuongeza kiwango cha sukari kwenye damu.

Anasema maua yanakuwa na mbegu za kiume, ambazo nyuki anazichukua na kuzichanganya na mwishowe inapatikana chavua ambayo sifa yake kubwa katika mwili wa binadamu kama ataitumia wanasayansi wanasema imeonyesha kuwa ikatumika ina uwezo kuongeza, kiwango cha mbegu za kiume.

Gabriel anasema ushauri ni kutumia bidhaa za nyuki mfululizo na kuwa ni utaratibu wa mlo wa kila siku au kutumia kama vile mafuta ya kupaka au jeli ili kupata matokeo chanya akiwashauri unapokuwa unatumia bidhaa za nyuki usitumie mara moja na kuacha, ili uone matokeo unatakiwa kutumia kama chakula tunasema utumie hizi bidhaa kama chakula usizitumie tu kama dawa siyo kwa muda mfupi.

"Inatakiwa utumie mara kwa mara na chavua inapatikana katika maua ya kiume na maua ya kike ili mmea uweze kuzaliana inabidi zile mbegu za kiume kutoka kwa mmea wa kiume ziende kwenye ua la kike moja kati ya kazi ya nyuki ni kufanikisha uchavushaji au 'pollination'.

Anasema pia chavua husaidia na kuimarisha afya ya ubongo kwa watu wenye matatizo ya kupoteza kumbukumbu na kwamba vifaa vya kuvunia mazao ya nyuki, amevibuni pia na vinamwezesha kuvuna sumu ya nyuki ambayo huuzwa kwa bei kubwa kwenye soko la dunia na vilevile bidhaa zinazovunwa hutunzwa kitaalamu, ili zisiharibike.

Anasema gramu moja ya jeli itokanayo na maziwa ya nyuki, huuzwa kati ya Sh. 30,000 hadi 50,000 na kwamba matumizi ya bidhaa hiyo ni katika kusaidia kupunguza kasi ya kuzeeka, ikiwamo mikunjo wa ngozi.

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

# Jihadhari usiwe kati ya 158,000 wanaokufa kila mwaka na dawa feki

• Fahamu namna ya kutambua, kukwepa



BAADA ya kazi za kutwa unahisi kuwa una maumivu ya kichwa. Unachokifanya ni kununua dawa za kutuliza maumivu kutoka kwa muuzaji wa duka lililoko mtaani. Kisha unameza mbili.

Lakini unajuaje iwapo vidonge hivyo ni halisi au ni bandia? Muuzaji siyo mtaalamu na kama ni duka halisi la dawa lililothibitishwa na mamlaka za uhakiki?

Hofu ya dawa feki ni tatizo kubwa Afrika na matokeo yake iwapo mtu atameza dawa zisizo na ufanisi ni kusababisha vifo.

Ni hatari kuwa kati ya vifo 64,000 na 158,000 vinavyohusishwa na ugonjwa wa malaria kila mwaka katika eneo la Kusini mwa Jangwa la Sahara na Tanzania ikiwepo, ni matokeo ya kutumia dawa feki.

Wagonjwa wanapewa dawa ambazo hazitafanya kazi mwilini au hazijatengenezwa kikamilifu kutibu ugonjwa husika ni hatari. Mambo hayaishii hapo zaidi ya watoto 250,000 duniani kote hufa kutokana na dawa feki kila mwaka.

Kwa mwaka uliopita pekee zaidi ya watoto 300 walikufa baada ya kutumia dawa feki za kikohozi au za kutuliza maumivu.

Lakini, hebu fikiria unanunua dawa hakuna kifungashio kinachoonyesha maelezo ya dawa na viwango au vipimo vya kutumia. Je, itakuwaje ikiwa umejaribu kutibu kichwa chako kwa kutumia dawa feki au bandia? Kama ripoti zinavyoeleza hakuna kupona matokea yake ni kifo.

Neno "bandia" humaanisha dawa ambazo zimeghushiwa kimakusudi na kwa ulaghai. Pia huitwa dawa zilizo chini ya kiwango au zilizoghushiwa, ni dawa ambazo ziko chini ya vipimo na viwango vya ubora ambavyo vimeidhinishwa na mamlaka za udhibiti wa dawa kitaifa na kimataifa.

Usizichanganye na dawa za asili hizo ni za bei nafuu, lakini zimethibitishwa kisayansi kuwa ni salama na zenye ufanisi na zina hati miliki.

Dawa feki au bandia zinazojulikana zaidi huwa ni dawa maarufu zaidi zikiwamo za kutuliza maumivu, za kutibu maambukizi mfano 'antibiotic' zipo za malaria, za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI VVU ambazo ni ARVs, kuna nyingine zinazoelezwa kuwa huongeza nguvu za kiume maarufu kama Viagra, kadhalika kuna za kupunguza uzito.

Dawa bandia, feki au za kughushi ni tatizo kubwa katika nchi nyingi za Afrika. Utafiti umeonyesha kuwa mataifa mengi yanayoendelea yana kiwango kikubwa cha dawa zisizo na viwango wala ubora

Kwa mfano, hadi asilimia 88.4 ya dawa za malaria katika baadhi ya masoko ya Afrika zimeripotiwa kuwa ni bandia.

### KUKABILIANA NAZO

Juhudi za kukabiliana nazo ni pamoja na kuimarisha ufuatiliaji wa serikali kuhusu dawa bandia. Kwa mfano, katika nchi nyingi za Kiafrika wafamasia wanapewa mafunzo ya kujenga uelewa wa dawa hizo na uwezekano wa kupenyezwa kwa dawa hizo katika mnyororo wa usambazaji.

Hii itawafanya wajiandae vyema kugundua dawa feki na kubadilishana taarifa na wagonjwa wao.

Hata hivyo, kuelimisha watumiaji wa mwisho wa dawa hawa ni wagonjwa, ni nguzo muhimu zaidi ya matumizi ya dawa salama.

Wagonjwa lazima wajue jinsi ya kukagua dawa kwa macho kwa kuangalia tarehe ya mwisho wa matumizi na alama zingine za utambulisho. Kuweza kutofautisha kati ya dawa bora na zile bandia kunaweza kuleta tofauti kati ya uhai na kifo. Zipo hatua tatu za kuchukua ili kubaini dawa bandia.

### DUKA RASMI

Kumbuka kununua dawa katika maduka yaliyosajiliwa, iwe maduka ya rejareja yaliyo na leseni na kwenye zahanati.

Hawa wanapaswa kubandika leseni zao kwenye kuta zao na unaweza kusoma kujiridhisha.

Wafamasia na wasaidizi wao wamefunzwa jinsi ya kushughulikia dawa. Wanawajibika kisheria na kimaadili kwa dawa zilizo chini ya udhibiti wao. Hii inamaanisha kuwa watapata bidhaa kupitia njia rasmi za dawa ambazo kuna uwezekano mdogo wa feki kupenyezwa.

> “Usinunue dawa kutoka kwa maduka ya mitandaoni. Katika nchi nyingi za Kiafrika, hakuna maduka ya dawa halali mtandaoni, mengi yanaelezwa ni feki.

### EPUKA MTANDAO

Usinunue dawa kutoka kwa maduka ya mitandaoni. Katika nchi nyingi za Kiafrika, hakuna maduka ya dawa halali mtandaoni, mengi yanaelezwa ni feki.

### KAGUA KWANZA

Ikague na kuihakiki dawa yako, hakikisha kukagua na kusoma kifungashio cha dawa.

Inapaswa kuwekewa lebo ya jina la bidhaa, maelezo ya mtengenezaji kama vile jina lao na anuwani ya mahali na tarehe ya mwisho wa matumizi.

Inapowezekana, angalia nambari ya kundi hii ni 'serial number' au msimbomilia au namba mistari 'barcode' ambayo inaweza kutumika kufuatilia ni lini na wapi bidhaa ilitengenezwa.

Ikiwa ni dawa ulizowahi kutumia hapo awali, jaribu kulinganisha na vifungashio vyote viwili,

Piga picha yake ikiwa unaitumia mara kwa mara kwa kulinganisha katika siku zijazo na hakikisha dawa imefungwa vizuri na iko sawa,

fungua kifurushi na uhakikishe.

Vidonge kwenye pakti, kwa mfano ni lazima kuhakikisha kwamba hakuna aliyejaribu kuvifungua na pia vidonge hivyo chunguza na hakikisha kwamba vinafanana bila kubadilika rangi, visiwe na madoadoa au ngozi yake isionekane yenye rangi tofauti, pia visiwe vimepasuka au kuwa na ukungu.

Baadhi ya mabaki ya poda katika vidonge yanakubalika, lakini haipaswi kuwa mabaki ama poda nyingi zaidi.

Hii inaweza kumaanisha kuwa vidonge havijabanwa vizuri, lakini pia haipaswi kuwa na harufu. Vidonge vinapaswa kung'aa na siyo kukutwa vimepasuka, kunata au kukunjamana.

### UKIBAINI FEKI

Ikibaini kuwa dawa yako ni feki, haina ubora au ni bandia, unapaswa kuripoti mara moja kwenye taasisi za udhibiti wa dawa au mdhibiti wa kitaifa wa dawa. Kila nchi barani Afrika ina mamlaka ya kitaifa ya kudhibiti dawa kama mamlaka huru au ndani ya wizara ya afya.

Ni vizuri pia kama umeitumia kusema athari ulizozipata hospitalini kwa wataalamu wa afya,

**BBC**

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Wafugaji hapa ndipo ilipo nyama bora, ukuaji kasi mifugo na gharama nafuu

UNAPOZUNGUMZIA malisho ya mifugo aina ya 'Cenchrus ciliaris' (jina la kitaalamu), unachoweza kusema ni hiki. Ndilo suluhisho la mfugaji kuachana na kusota kutafuta majani na kutumia gharama kubwa kulisha wanyama.

Watu wengi wamekuwa wakitegemea kuwalisha wanyama wao pumba, mashudu ya alizeti na pamba au uduvi na soya kwa kuku, bata na jamii ya ndege ili kuwaongezea protini.

Lakini ujio wa Cenchrus ilirahisisha hasa kwa wafuga ng'ombe, farasi, kondoo na mbuzi gharama zimepungua kwa sababu malisho hayo yanatumia gharama kiduchu na kuongeza uzalishaji wa maziwa na nyama kwa muda mfupi.

Ni aina ya majani au malisho ya mifugo ambayo yametafitiwa kisayansi na kubainika kuwa ni bora na yana virutubisho vingi muhimu kwa ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda na farasi.

Ofisa Mtafiti Mifugo kutoka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Nchini (TALIRI), Jovith Kajuna, anasema hayo jijini Dar es Salaam, anapozungumza na Nipashe, hivi karibuni.

Anasema kuwa majani hayo yanaota na kustawi katika maeneo mengi yenye mvua nyingi, au ya wastani na nyanda kame hapa.

Jovith anazungumzia umuhimu wa malisho haya kwa mifugo akisema yana virutubisho vingi muhimu vinavyoongeza uzalishaji maziwa kwenye ng'ombe na mbuzi, kondoo na ukuaji wa haraka na bora wa mifugo pamoja na kuboresha ladha na ubora wa nyama.

" Si hayo tu, pia kwa mfanyabiashara na mfugaji, malisho haya yana faida nyingi yanapokuwa yameyastawishwa katika shamba kwa sababu yana uwezo wa kuendelea kutoa mazao ya mbegu na nyasi kwa ajili ya kutengeneza malisho ya 'hei'."

Mtafiti huyo anaeleza kuwa hei au silages ni aina ya malisho makavu yaliyohifadhiwa ambayo yanaweza kukaa kwa muda wa miaka 10-15 kabla ya kupanda upya shambani.

"Ukifanya ulinganifu wa gharama za uzalishaji wa malisho aina ya Cenchrus ciliaris na mkulima aliyepanda mahindi shambani au mpunga , utagundua kuwa mkulima aliyepanda mahindi analazimika kila mwaka kuandaa shamba upya, kununua mbegu na kupanda, kupalilia ambavyo vyote vinamwingiza kwenye gharama zinazojirudia tofauti na aliyepanda malisho aina hii," anasema Jovith.



Ndiyo majani ambayo wataalamu TALIRI wanawashauri wafugaji kuyatumia kuongeza tija.
**PICHA: BEATRICE PHILEMON**

> Tunaomba Watanzania watumie fursa hii ya kupanda malisho haya, wakitaka mafunzo jinsi ya kuyatunza, kuyahudumia, wataalamu kutoka TALIRI wapo tayari kutoa huduma ya kupanda.



Mbali na hilo, malisho haya yanampa mkulima au mfugaji fursa ya kupata faida itokanayo na mbegu ambazo zinauzwa kwa sasa Shilingi 20,000 kwa kilo katika taasisi za serikali kama TALIRI na kati ya shilingi 50,000 hadi shilingi 80,000 kwenye maeneo ya watu binafsi.

Lakini pia baada ya kuvuna mbegu unaweza kuvuna nyasi, ukazikausha na kufunga marobota ya hei ambazo zinauzwa kati ya Shilingi 3,000 hadi shilingi 5,000 kwenye taasisi za umma au zaidi kwa wauzaji binafsi.

Mtafiti huyo anasema malisho yaliyohifadhiwa hutumika kumsaidia mfugaji kulisha mifugo yake hususani wakati wa kiangazi, au kipindi cha ukame ambapo kuna upungufu mkubwa wa malisho au majani.

Anasifia uzalishaji wa malisho aina ya Cenchrus ciliaris kuwa umekuwa ni fursa kubwa kibiashara ndani na nje ya nchi, kwa sababu huhitajika na wafugaji wengi kwa kuwa wengi wamehamasika kufuga kibiashara tofauti na ilivyokuwa hapa zamani.

Aidha, idadi ya ng'ombe wa wanaofungwa ndani wakiwemo wa maziwa na wa kunenepesha kwa ajili ya nyama nayo imeongezeka.

Kwa upande wa hei ambayo ni majani makavu, pia masoko ya nje yameongezeka kwa kasi na kwamba Tanzania haina uwezo mkubwa wa kuzalisha ikilinganishwa na mahitaji ya soko katika mataifa ya Comoro, Shelisheli na Congo.

Mbali na hilo, Jovith anasema zipo fursa za kununua marobota ya hei katika eneo moja kwenda sehemu nyingine yenye uhitaji kulingana na wafugaji.

"Tunaomba Watanzania watumie fursa hii ya kupanda malisho haya, wakitaka mafunzo jinsi ya kuyatunza, kuyahudumia, wataalamu kutoka TALIRI wapo tayari kutoa huduma ya kupanda," anasema mtafiti huyo.

Anasema malisho haya yanawahakikishia kuondoa tatizo la majani kwa mifugo yao na ndiye mkombozi kiuchumi kwa vile wanaweza kuuza nje na kupata fedha za kigeni.

"Mifugo yao inakuwa na uhakika wa malisho, nyama na maziwa bora na mengi. Ziada wanauza nje , yote hayo yakikuza uchumi na maendeleo ya sekta ya mifugo na kilimo." Anaongeza,

Ili kusaidia wananchi kujua faida za malisho haya, hivi karibuni TALIRI ilishiriki katika maonyesho ya Sabasaba jijini Dar es Salaam na wataalamu wa taasisi hiyo waliwaelimisha na kuwafunza wananchi kuhusu uwekezaji huo wenye tija kwenye kilimo cha Cenchrus ciliaris.

**UZALISHAJI**

Jovith anasema mkulima au mfugaji ambaye yupo tayari kujikita kupanda malisho haya kwa ajili ya biashara na mifugo anatakiwa kufahamu kuwa , hekari moja inatoa kati ya marobota 200 hadi 300 ya malisho hayo lakini pia kutegemea na aina ya udongo.

Halikadhalika anaongeza kuwa maeneo yaliyowekwa mbolea uzalishaji unaweza kufikia marobota 450 kwa hekari moja.

HABARI DODOMA



## Kampuni binafsi zinazowekeza kwenye afya kusaidiwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde amesema serikali itaendelea kuzisaidia kampuni binafsi ambazo zinawekeza kwenye taasisi za umma ikiwamo katika sekta ya afya, elimu na kilimo.

Mavunde alisema hayo juzi alipokuwa akizindua mtambo wa umeme jua wa Sola Sun King, uliofugwa kwenye jengo la wodi ya mama na mtoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Alisema, serikali itaendelea kuthamini mchango mkubwa unaofanywa na kampuni binafsi zinazowekeza kwa ajili ya kuhudumia jamii kama vile kwenye vituo vya afya shule, sekta ya kilimo na nyinginezo.

"Kwa kitendo hiki ambacho mmekifanya nyinyi kampuni ya Sola ya Sun King ya kuwekeza umeme kwenye hospitali hii ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma ni kitendo cha kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan katika kuwasogezea huduma za kijamii na hasa suala la umeme kwenye maeneo kama haya ya wodi za mama na mtoto.

"Hivyo niziombe kampuni zingine kufungua milango ya kuwafikia maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuwahudumia wahitaji wanayohitaji kupitia miundombinu kama kwenye sekta ya elimu, afya ufugaji uvuvi na kwenye kilimo pia," alisema

Mkurugenzi wa kampuni ya Sun King Lucy Merinyo, alisema wameweka mtambo wa umeme huo wa jua kwa ajili ya kuwasaidia kinamama, watoto na wajauzito pia kwenye huduma za upasuaji wanaolazwa katika hospitali hiyo.

"Umeme huo wa Sola Sun King una uwezo wa kufanya kazi hata kama hakuna jua au wakati mvua inanyesha kwa saa 10 umeme huo utakuwa ukifanya kazi," alisema.

Hata hivyo, alisema kampuni hiyo yenye uzoefu wa miaka 13 nchini imefanikisha kusongeza huduma za umeme kwenye mikoa 10 na kuwezesha kutoa ajira 3,500 na kati ya hao walioajiriwa ni 400 na hadi kufikia mwaka 2023 watakuwa wameajiri wafanyakazi 6,000 wa kudumu.

# Utafiti wabaini Dodoma kuwa na madini aina nyingi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

UTAFITI uliofanywa na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) umebaini kuwa Dodoma inaongoza kuwa na aina nyingi za madini yanayopatikana nchini.

Akiwasilisha taarifa hiyo juzi jijini hapa, Meneja jiolojia kutoka (GST), Maswi Solomon, alisema kuwa utafiti huo umeonesha miongoni mwa madini aina tano ya kimkakati, aina nne yako katika mkoa wa Dodoma.

Alisema mkoa huo ni maarufu kwa upatikanaji wa miamba yenye madini ya lithium, chrysoprase, chuma, nikeli, urania na jasi.

Aidha, taarifa hiyo imeonyesha kuwa kuna madini ya yoderite yanayopatikana mlima wa Mautya wilayani Kongwa na imebainika kuwa madini hayo hadi sasa yanapatikana Tanzania pekee duniani kote.

Akipokea taarifa ya utafiti huo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema taarifa hiyo itakuwa ni nyenzo itakayosaidia kuutangaza mkoa kimkakati husasani katika uwekezaji wa sekta ya madini.

"Nawashukuru sana GST kwa kuwasilisha kitabu hiki na ramani inayoonyesha madini katika Mkoa wa Dodoma, ni taarifa muhimu sana ya kuvutia wawekezaji kwa kuwa imeainisha aina ya madini na eneo yanapopatikana," alisema Senyamule.

Aidha, Senyamule alitoa wito kwa jamii kutumia taasisi hiyo ya serikali katika kufanya utafiti wa ardhi kabla ya kuanza kwa ujenzi wa ghorofa ili kuepuka madhara.

Mbali na hayo mkuu wa mkoa huyo alitoa rai kwa taasisi hiyo kushirikiana na bonde la Wami Ruvu katika kuendeleza tafiti za wingi wa maji katika bonde hilo kwa kuwa taasisi ya GST imethibitisha kuwa na vifaa na utaalamu wa kutosha.

Alisema Jiolojia ya Mkoa wa Dodoma imegawanyika katika makundi manne huku sehemu kubwa ikiwa ni ile ya kundi la miamba ya Archean ya Dodoma na Nyanzian ambayo baadhi yake ni maarufu kwa upatikanaji wa madini ya dhahabu, ila kwa Dodoma miamba hii ina madini ya chuma, urani, nikeli na lithium.

Aina ya pili ni miamba ya Usagaran ambayo ni maarufu kwa uwapo wa madini ya vito, chuma na shaba.

Aina ya tatu ya miamba ile ya ukanda wa Neoproterozoic Mozambique Mobile Belt inayopatikana wilaya za Kondoa, Mpwapwa na Kongwa na maarufu kwa madini ya shaba na vito hasa rubi.

Nne ni neogene inayopatikana katika maeneo ya Farkwa na Mpondi Wilaya ya Chemba, Gonga na Kondoa.




Mkurugenzi wa kampuni ya umeme jua ya Sola Sun King Home 8000, Lucy Bonaventure, akipanda mti kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kati ya 50 iliyopandwa baada ya kampuni hiyo kutoa msaada wa mtambo wa umeme jua katika jengo la wodi ya mama na mtoto jana. Wa tatu kulia ni Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, (wa tatu kushoto) Meneja wa Kanda, Rweyemamu Protace. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Atoa wiki mbili shule sekondari ipatiwe madawati

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Singida, Martha Mlata, ametoa wiki mbili kwa Halmashauri ya Itigi wilayani Manyoni kupeleka madawati katika shule mpya ya Sekondari Mwamagembe ili wanafunzi waanze masomo.

Hatua ya mwenyekiti huyo kutoa agizo hilo ilifuatia baada ya kuelezwa kuwa wanafunzi wanaofaulu kwenda sekondari kutoka katika Kata ya Mwamagembe wanalazimika kutembea umbali wa kilometa 70 kwenda kusoma katika kata nyingine ya Rungwa ambayo ndiyo ina sekondari.

Mlata alitoa agizo hilo jana akiwa na Kamati ya Siasa ya Mkoa baada ya kutembelea Shule ya Sekondari ya Mwamagembe iliyojengwa kwa nguvu za wananchi kwa kusaidiwa na halmashauri na wadau mbalimbali, lakini tangu mwaka 2019 haitajaanza kutumika kwasababu hakuna madawati.

"Natoa agizo kwa halmashauri ipeleke madawati katika shule hiyo ya sekondari kabla ya Agosti 15, mwaka huu ili wanafunzi wanaosoma kata ya Rungwa warudi kusoma Kata ya Mwamagembe karibu na wazazi wao," aliagiza.

Mlata alisema kitendo cha wanafunzi wanaotoka kata ya Mwamagembe kutembea umbali mrefu kwenda kusoma Kata ya Rungwa kunafanya wanafunzi wa kike kukata tamaa ya kusoma na kubaki kuwa wake za watu au kufanya kazi za ndani jambo ambalo serikali ya CCM haiwezi kukubali.

Alisema alichobaini ni ukanda huo ambao una wafugaji wengi hakuna jitihada za madhubuti zilizochukuliwa kuhakikisha watoto wanapata elimu na kuielekeza serikali kuu kuongeza nguvu katika kujenga shule ili watoto wengi wapate fursa ya kusoma.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mwamagembe kwenye mkutano wa hadhara alisikitika kukosekana kwa huduma ya umeme wakati nguzo zipo na kuagiza viongozi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), kufika katika kijiji hicho kutafuta ufumbuzi wa changamoto hiyo.

Diwani wa Kata ya Mwamagembe, Jonathan Dulle, alisema kutokana na kukosekana kwa sekondari katika kata hiyo kwa muda mrefu wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na sekondari kutokana na umbali mrefu wa kwenda kusoma Kata ya Rungwa, wengi hawaendi shule.

Dulle alitoa mfano mwaka huu kati ya wanafunzi 96 waliofaulu na kuchaguliwa kuendelea na masomo ya sekondari wanafunzi sita tu ndio wanaendelea na masomo, 44 wamehama na wanafunzi 46 hawajulikani waliko hadi sasa.

Naye, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Itigi, Hussein Simba, alimwahidi Mwenyekiti wa CCM Mkoa kuwa atahakikisha madawati katika shule hiyo yanapelekwa kabla ya Agosti 15, mwaka huu.

TANGAZO

BANK OF AFRICA
BMCE GROUP

# TAARIFA YA FEDHA YA BANK OF AFRICA TANZANIA LIMITED YA 30 Juni 2023

Taarifa ya fedha ya Benki iliyochapishwa kwa mujibu wa kifungu na 7 na 8 cha sheria ya Benki na taasisi za fedha ya mwaka 2014

## MUHTASARI WA TAARIFA ZA FEDHA

### MIZANIA

| | Mikopo Halisi | Amana za Wateja | Mikopo Chechefu |
|---|---|---|---|
| Mabadiliko | ↑ 14% | ↑ 22% | ↓ -2.8% |
| Jun 23 | TZS 452.6B | TZS 549.1B | TZS 1.55% |
| Jun 22 | TZS 395.9B | TZS 448.8B | TZS 4.3% |

### MAPATO

| | Faida (Kabla ya Kodi) | Mapato Yasiyo ya Riba | Mapato ya Riba |
|---|---|---|---|
| Mabadiliko | ↑ 88% | ↑ 13% | ↑ 23% |
| Jun 23 | TZS 8.9B | TZS 12.6B | TZS 33.1B |
| Jun 22 | TZS 4.8B | TZS 11.1B | TZS 26.9B |


BANK OF AFRICA
BMCE GROUP
WAKALA
Benki Karibu Yako.

HUDUMA KARIBU YAKO.
Toa na tuma pesa kupitia Wakala wetu

Kanda ya Pwani
Dar es alaam
Morogoro
Mtwara
Zanzibar

Kanda ya Kaskazini
Arusha
Moshi

Kanda ya Ziwa
Mwanza
Kahama

Kanda ya Kusini
Mbeya
Tunduma

Kanda ya Kati
Dodoma




*Vigezo na masharti kuzingatiwa


## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI

(Kiasi kwa millioni shillingi)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ongezeko la thamani | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2023** | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 50,500 | 22,242 | 11,796 | 6,425 | 90,963 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 6,031 | - | 6,031 |
| Faida / (Hasara) ya mabadiliko ya thamani | | | - | (4,272) | (4,272) |
| Salio la mwisho wa mwaka 2023 | 50,500 | 22,242 | 17,827 | 2,153 | 92,722 |
| Mwaka Uliopita 2022 | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2022 | 50,500 | 22,242 | 6,493 | 2,671 | 81,906 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 5,303 | - | 5,303 |
| Faida / (Hasara) ya mabadiliko ya thamani | - | - | - | 3,754 | 3,754 |
| Salio la mwisho wa mwaka 2022 | 50,500 | 22,242 | 11,796 | 6,425 | 90,963 |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30.06.2023

(Kiasi kwa millioni shillingi)

| | Robo ya Mwaka sasa iliyoisha 30 Juni 23 | Robo ya Mwaka Linganishi(Mwaka Uliopita) 30 Juni 22 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Juni 23 | Limbikizo mwaka linganishi 30 Juni 22 |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 17,105 | 14,317 | 33,065 | 26,913 |
| 2. Gharama za Riba | (7,361) | (5,573) | (14,646) | (10,391) |
| **3. Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **9,744** | **8,744** | **18,419** | **16,522** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 41 | (862) | 174 | (2,674) |
| **6. Mapato Yasiyo ya Riba:** | **5,370** | **3,987** | **12,594** | **11,141** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1,870 | 1,103 | 2,674 | 2,172 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 3,366 | 2,457 | 6,458 | 5,124 |
| 6.3 Gawio | - | 28 | - | 28 |
| 6.4 Mapato Mengine | 134 | 399 | 3,462 | 3,817 |
| **7. Gharama Zisizo za Riba:** | **(11,386)** | **(10,027)** | **(22,252)** | **(20,232)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (5,263) | (4,193) | (9,926) | (8,072) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (895) | (424) | (1,676) | (892) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (5,228) | (5,410) | (10,650) | (11,268) |
| **8. Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **3,769** | **1,842** | **8,935** | **4,757** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | (1,199) | (552) | (2,904) | (1,427) |
| **10. Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **2,570** | **1,290** | **6,031** | **3,330** |
| 11. Idadi ya Waajiriwa | 300 | 296 | 300 | 296 |
| 12. Mapato kwa Hisa | 277,680 | 220,559 | 325,815 | 220,559 |
| 13. Idadi ya Matawi | 19 | 19 | 19 | 19 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.3% | 0.8% | 1.6% | 1.0% |
| Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 11.2% | 6.0% | 13.2% | 7.8% |
| Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 75.3% | 78.8% | 71.8% | 73.1% |
| Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.0% | 6.5% | 5.7% | 6.1% |

## WARAKA WA MIZANIA KWA TAREHE 30.06.2023

(Kiasi kwa millioni shillingi)

| | Robo mwaka sasa 30 Juni 23 | Robo mwaka Mwaka linganishi 31 Machi 23 |
|---|---|---|
| **A.MALI** | | |
| 1.Fedha Taslimu | 25,213 | 17,905 |
| 2.Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 39,679 | 52,366 |
| 3. Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 147,796 | 134,939 |
| 4. Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 7,580 | 10,984 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 7,210 | 8,668 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 38,615 | 96,010 |
| 10. Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 452,645 | 416,636 |
| 12. Mali Nyingine | 14,010 | 17,087 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | 1,894 | 1,894 |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Haki ya matumizi ya mali | 7,280 | 7,459 |
| 16. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 8,782 | 8,774 |
| **17. JUMLA YA MALI** | **750,704** | **772,722** |
| **B.DHIMA** | | |
| 18.Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | | |
| 19.Amana za Wateja | 68,083 | 82,342 |
| 20.Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 471,352 | 478,471 |
| 21.Amana Maalumu | - | - |
| 22. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 77,756 | 80,063 |
| 23. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 24. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 77 | 77 |
| 25. Madeni ya kukodisha | 1,732 | 1,560 |
| 26. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 8,123 | 8,288 |
| 27. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 28. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | - | - |
| Zitakazolipwa Baadae | 3,583 | 4,060 |
| 29. Dhima Nyingine | 16,408 | 16,451 |
| 30. Madeni | 10,868 | 10,868 |
| **31. JUMLA YA DHIMA** | **657,982** | **682,180** |
| **32. MALI/(DHIMA) HALISI (17 kutoa 31)** | **92,722** | **90,542** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 33. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 50,500 | 50,500 |
| 34. Akiba ya Mtaji | 22,242 | 22,242 |
| 35. Mapato Yaliyobakizwa | 11,796 | 11,796 |
| 36. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 6,031 | 3,461 |
| 37. Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 38.Tengo la ongezeko la thamani | 2,153 | 2,543 |
| 39. Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **40. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **92,722** | **90,542** |
| 41. Dhima Zisizo Dhahiri | 149,944 | 99,582 |
| 42. Mikopo Chechefu | 7,164 | 7,046 |
| 43. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 10,948 | 10,789 |
| 44. Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 12.4% | 11.7% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1.55% | 1.6% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 75.1% | 66.7% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 60.3% | 53.9% |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 87.1% | 86.3% |
| (vi) Ongezeko la Amana | -1.7% | -1.2% |
| (vii) Ongezeko la Mali | -2.8% | -0.4% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30.06.2023

(Kiasi kwa millioni shillingi)

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Juni 23 | Robo Mwaka iliyopita 31 Machi 23 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30 Juni 23 | Limbikizo la Mwaka Linganish (Mwaka Uliopita) 30 Juni 22 |
|---|---|---|---|---|
| **I.Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 3,769 | 5,166 | 8,935 | 4,758 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| - Hasara Katika Mali | 2,088 | 1,779 | 3,867 | 6,489 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | - | - | - | (83,303) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (36,936) | 6,490 | (30,446) | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (23,685) | (2,286) | (25,971) | 82,976 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (513) | (104) | (617) | (156) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 2,194 | (1,933) | 261 | (848) |
| - Kodi Iliyolipwa | (348) | (348) | (696) | (287) |
| -Kiwango cha chini cha tengo la ziada | (131) | (9,740) | (9,871) | (1,427) |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(53,562)** | **(976)** | **(54,538)** | **8,202** |
| | | | - | - |
| **II.Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | - | - |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | 28 |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1,348) | (1,340) | (2,688) | 3,350 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (12,857) | - | (12,857) | -17,702 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | 1,867 | 1,867 | 16,890 |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(14,205)** | **527** | **(13,678)** | **2,566** |
| **III.Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | 107 |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **107** |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (67,767) | (449) | (68,216) | 10,875 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 152,812 | 153,261 | 153,261 | 113,277 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 85,045 | 152,812 | 85,045 | 124,152 |

| Jina na Cheo: | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Adam Mihayo (Ofisa Mtendaji Mkuu) | .............................. | 28 Julai 2023 |
| Derick Lugemala (Mkuu wa Fedha) | ................................. | 28 Julai 2023 |
| Alex Kibiki (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | ................................. | 28 Julai 2023 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| Nehemiah Mchechu (Mwenyekiti) | ................................. | 28 Julai 2023 |
| Moremi Marwa (Mkurugenzi) | ................................. | 28 Julai 2023 |

**As strong as a group. As close as a partner.**




BANK OF AFRICA
BMCE GROUP

## TAARIFA FUPI YA GHARAMA ZA HUDUMA ZETU

| Type of Charge | Product | Charges TZS | FCY (USD, EUR,GBP) |
|---|---|---|---|
| Opening Balance | Corporate Current Account | 250,000 | 500 |
| | SME Current Account | 100,000 | 100 |
| | Personal Current Account | 100,000 | 50 |
| | Faidika Savings Account | 15,000 | 15 |
| | Smart Junior Investor Account | 50,000 | USD 50/ GBP 20/ EUR 15 |
| Minimum Operating Balance | Corporate Current Account | 100,000 | 250 |
| | SME Current Account | 50,000 | 50 |
| | Personal Current Account | 5,000 | 5 |
| | Faidika Savings Account | 10,000 | 10 |
| | Smart Junior Investor Account | 25,000 | Equivalent to TZS |
| | Penalty Below Minimum balance | 12,000 | Equivalent to TZS |
| Minimum Interest Earning Balance | Faidika Savings Account | 1,200,000 | 1,200 |
| | Smart Junior Investor Account | 1,200,000 | 1,200 |
| Ledger Fee | Corporate Current Account | 30,000 | Equivalent to TZS |
| | SME Current Account | 15,300 | 15 |
| | Personal Current Account | 10,300 | 10 |
| | Faidika Savings Account | 1,800 | Equivalent to TZS |
| | Smart Junior Investor Account | nil | nil |
| Withdrawal Charges Over the Counter | **For Corporate & SME** | | |
| | < 15 Million | 2,500 | 1.2% of the amount min 5 |
| | > 15 Million | 1% of the amount max 50,000 | |
| | **For Individuals** | | |
| | < 10 Million | 2,000 | 1% of the amount min 5 |
| | > 10 Million | 0.12% of the amount max 50,000 | |
| Cheques | Cheque Book Issuance-100 leaves | 67,500 | Equivalent to TZS |
| | Cheque Book Issuance-50 leaves | 34,000 | Equivalent to TZS |
| | Cheque Book Issuance-25 leaves | 34,000 | 15 USD/11 EUR/15 GBP |
| | Counter Cheque Leaf for Corporate & SME | 18,000 | 16 |
| | Counter Cheque Leaf for Individuals | 20,000 | Equivalent to TZS |
| | Stop Payment Local Cheque | 1% of total value with min 50,000 and max 250,000 | Equivalent to TZS |
| Statements | Account Statements on Banking Hall per month | 2,000 per page max 100,000 | Equivalent to TZS |
| | E-Statements (Daily, weekly, Monthly, Quarterly) | Free | Free |
| Standing Order | To other Banks | 5,000+ TISS Charges total 15,000 | 15 |
| | Within the Bank | 5,000 | 5 |
| Telegraphic Transfers | TISS (Incoming transfers) | Free | Free |
| | TISS (Outgoing transfers) | 10,000 | Equivalent to TZS |
| | Outward TT- Customer | Equivalent to FCY | $ 54 via Internet Banking, $ 60 without Internet Banking |
| Other Charges | Account Closure | 50,000 | 50 |
| | Dormant Account Activation | Free | Free |
| **TRADE SOLUTIONS** | | | |
| Letters of Credit | **Import LC:** | | |
| | Opening L/C | Equivalent to FCY | 1% pq min 250 |
| | Swift Charges | Equivalent to FCY | 60 |
| | L/C acceptance | Equivalent to FCY | 0.10% |
| | **Export LC:** | | |
| | Confirmation charge - unsecured | Equivalent to FCY | 1.2% min 300 per qtr |
| | Document verification | Equivalent to FCY | 150 |
| | Amendments | Equivalent to FCY | 120 flat fee |
| Bonds and Guarantees | Bid Bond | Unsecured 3.6%; Secured 3%; Cash cover 0.6% per qtr | Equivalent to TZS |
| | Performance bonds | Secured 3%; Full cash cover 0.6% per qtr | Equivalent to TZS |
| | Advance payment | Secured 3%; Full cash cover 0.6% per qtr | Equivalent to TZS |
| | Other guarantees | Secured 3%; Full cash cover 0.6% per qtr | Equivalent to TZS |
| **DIGITAL BANKING** | | | |
| Internet Banking | Subscription | Free | Free |
| | Maintanance Fee | Free | Free |
| | E-Statements | Free | Free |
| | Outward TT | Equivalent to FCY | $54 |
| Mobile Banking | Subscription | Free | n/a |
| | Maintanance Fee | Free | n/a |
| | Balance Enquiry | 200 | n/a |
| | Mini-Statement | 300 | n/a |
| | Full- Statement | 500 | n/a |
| | Fund transfer to other Banks | 10,000 | n/a |
| | Fund transfer to other accounts within BOA | 450 | n/a |
| | Bank to wallet | 1,000 - 49,999 = 2,500<br>50,000 - 99,999 = 3,000<br>100,000 - 199,999 = 3,500<br>200,000 - 499,999 = 5,500<br>500,000 - 1,000,000 = 7,500<br>Above 1,000,000 = 8,500 | n/a |
| | Wallet to Bank | nil | n/a |
| | Forex Rate request | 300 | n/a |
| | Utility Bills Payment | Free | n/a |
| | Airtime Purchase | Free | n/a |
| | SMS Alert | 2500 per Month | n/a |
| Loans | Loan Application Fee | 0.12% of the principal amount minimum TZS 150,000 | Equivalent to TZS |
| | Base/Prime Lending rate | 17% | 8% |

| Cards | | SESAME MAUVE (PURPLE) | SESAME MAUVE (PURPLE) | VISA BLUE | VISA ELITE | VISA GREEN |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Joining Fees | 0 | 0 | 0 | 0 | 6000 |
| | Card Replacement | 24000 | 24000 | 24000 | 25000 | 6000 |
| | PIN Re-issue | 7500 | 7500 | 6000 | 7500 | 6000 |
| | Block card by Bank | 2500 | 2500 | 2000 | 2000 | 2000 |
| | ATM Cash withdrawal us-on-us | 1300 | 1300 | 1500 | 1500 | 1500 |
| | ATM Cash withdrawal Domestic us-on-them | 1000-99999=1500<br>100000-400000=1700 | 1000-99999=1500<br>100000-400000=1700 | 3000 | 3000 | 3000 |
| | ATM Balance enquiry us-on-us | 400 | 400 | 300 | 300 | 300 |
| | ATM Balance enquiry Domestic us-on-them | 400 | 400 | 600 | 600 | 600 |
| | Cash advance us-on-us | 300 | 300 | 300 | 300 | 300 |
| | Cash advance Domestic us-on-them | 1500 | 1500 | 1500 | 1500 | 1500 |
| | Mini statement us-on-us | 400 | 400 | 600 | 600 | 600 |
| | Mini statement BOA network | 400 | 400 | 1800 | 1800 | 1800 |
| | Failed transactions (Insufficient funds) | 900 | 900 | - | - | - |

BANK OF AFRICA
BMCE GROUP

Benki kidijitali na
B-Mobile
*150*13#




Hamisha pesa
Hamisha kwenda benki na mitandao yote ya simu

Nunua LUKU

Lipia king'amuzi

Salama
Loki kwa sura au alama za vidole

Bili ya maji

Nunua vocha

Pakua kutoka App Store Google Play au Piga *150*13#




Umoja wa Vijana wa CCM wakiongozwa na Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Mjini Zanzibar, Hussein Ayoub Idd (kulia), baada ya kufika Jaws Corner kijiwe maarufu cha ACT-Wazalendo kwenye Mjimkongwe wa Zanzibar. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# ACT-Wazalendo yatoa neno Pennyroyal kufutiwa kibali

**Na Mwandishi wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimesema kitendo cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufuta kibali cha umiliki wa ardhi kwa kampuni ya Pennyroyal Resort kina madhara makubwa kiuchumi na maendeleo ya sekta ya utalii Zanzibar.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, Ismail Jussa Ladhu, alisema hayo alipokuwa akihutubia mkutano wa hadhara wa chama hicho uliofanyika uwanja wa Chwaka Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema, kampuni hiyo kupitia mradi wake wa Bluu Amber walikuwa wajenge hoteli yenye hadhi ya nyota tano, lakini ghafla wamefutiwa kibali cha umiliki wa ardhi mwaka 2022.

Alisema kampuni hiyo sasa imeamua kufungua kesi katika mahakama ya kimataifa ya Benki ya Dunia ikidai kulipwa fidia ya Shilingi trilioni 2.5 sawa na bajeti ya mwaka mmoja ya Serikali ya Zanzibar.

"Sasa leo unakwenda kudaiwa fidia ya shilingi trilioni 2.5... patamu, lakini sasa iliyoshtakiwa siyo Zanzibar bali imeshtakiwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, sasa tangu limeripotiwa hili kumezuka malalamiko kutoka Tanganyika wanasema mambo ya ardhi na uwekezaji siyo ya muungano mbona inashtakiwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano," alisema Jussa.

Alisema kampuni ya Pennyroyal kutoka Uingereza ilijitokeza kuwekeza Zanzibar katika eneo la Mbuyu Tende Mkoa wa Kaskazini Unguja na kununua hekari 411 ya ardhi na kupewa kibali cha matumizi ya ardhi na umiliki na serikali na kuanza ujenzi wa hoteli na nyumba za makazi kabla ya kufutiwa kibali hicho.

Hata hivyo, alisema kwamba mwaka 2022 kiongozi mmoja alitaka kumegewa hekari 80 katika eneo hilo ili awape wawekezaji wa kampuni mbili kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

"Mradi huu ulikuwa ufunguwe mlango wa utalii wa Zanzibar kimataifa, kuongeza ajira na kukuza uchumi Zanzibar, leo watu wamepoteza ajira na sasa tujiandae kubeba deni la fidia la trilioni 2.5 kwa nchi maskini kama Zanzibar," alisema.

Alisema kesi hiyo imeshaanza kusikilizwa Uingereza dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa vile ndiyo inayohusika katika mambo ya nje ya kimataifa baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964.

Alisema kama Serikali ya Muungano itagoma katika deni hilo, Zanzibar ipo katika hatari ya kutaifishwa mali zake kutokana na mwelekeo mbaya wa kesi unavyoendelea nchini Uiengereza.

Kadhalika, alitaka serikali ijifunze kuheshimu utawala wa sheria hasa mikataba ya uwekezaji ili kuepusha hasara ambazo hazina msingi katika kukuza uwekezaji na maendeleo ya sekta ya utalii.

Akizungumzia miradi ya ujenzi wa barabara Zanzibar, Jussa alisema imekuwa ikifanyika bila ya kutangazwa zabuni kinyume na sheria ya ununuzi na ushindani iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Hata hivyo, alisema Chama cha ACT kitakapochukua madaraka mwaka 2025, mikataba yote itapitiwa upya na viongozi waliohusika na ufisadi uliofanyika watafunguliwa mashtaka mahakamani.

Aidha alisema kuna kampuni moja kutoka Uturuki ndiyo imekuwa ikipewa kazi zote za ujenzi wa barabara bila ya kutangazwa zabuni jambo ambalo halikubaliki katika misingi ya utawala bora.

Akigusia ujenzi wa uwanja wa Amani, Jussa alisema gharama zinazotumika ni kubwa ikilinganishwa na kazi inayofanyika.

Alisema wakati Serikali ya Jamhuri ya Muungano imetangaza kutumia shilingi bilioni 31 kukarabati uwanja wa Benjan Mkapa wenye uwezo wa kuchukua watu 60,000 wakati SMZ imetangaza kutumia Sh. bilioni 51 kukarabati Uwanja wa Amani wenye uwezo wa kuchukua watu 12,000.

Alisema kazi ya ujenzi wa uwanja huo imetolewa kwa kampuni iliyopewa kazi bila ya kutangazwa zabuni.

Pia hoja zinazotolewa na serikali kuwa wametumia sheria ya dharura ili uwanja huo ukarabatiwe kwa ajili ya sherehe za miaka 60 ya Mapinduzi mwaka 2024 hazina msingi wowote kwa vile kila kiongozi na mwananchi anajua kuwapo kwa sherehe hizo.

Chama cha ACT-Wazalendo kimekuwa kikitumia muda mwingi kujadili vitendo vya ufisadi na ubadhirifu licha ya kuwamo katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AIKA CAROLINE LADISLAUS JOHN** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA YA USAJILI T 540 DGS – TOYOTA RAUM. ENGINE NAMBA INZB784071.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **KW/RB/3076/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SUNDAY KILIAN BAHARIA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA YA USAJILI T 535 DSU – TOYOTA PREMIO. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **KW/RB/3075/2023**.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**INNOCENT FRANK LOVELAND** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 152 ACR – TOYOTA HILUX.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DSM/PHQ/RB/178937/2023**.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SALEHE ABDALA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA YA USAJILI T 121 CPE – SUZUKI CARRY. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/URA/RB/256138/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**CALIST VIRGIL MUSHI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S4090-0251 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia NGARENARO SEKONDARI mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya polisi: DAR/CHU/RB/212606/2023.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 55 LA 2023**
**ZO SPACES LIMITED.............MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**

- **GORICH HUB LIMITED**
- **OTTUMAN JOHN CHINGO......... MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**
**GORICH HUB LIMITED**
**OTTUMAN JOHN CHINGO.........POPOTE ULIPO/MLIPO**

**ZO SPACES LIMITED** amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni Mwananyamala. Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 16/08/2023 saa 03:00 asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 24 Mwezi 07...2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

## KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA

**BRUNO SURUMBU LAGWEN** anatangaza kupotelewa na kadi ya Trekta yenye namba za usajili T522CNB aina ya New Holland, chasis namba 2249185, Engine namba 115946N.
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MAN/BAB/RB/255121/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GASTON BLASTO MAKUNDI** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA YA USAJILI MC 507 DCK AINA YA TVS-HLX. CHASSIS NAMBA MD625AF43M1K02544. CHASSIS NAMBA DF4KM1002320. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/CEN/RB/356065/2023.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI MADOGO NA. 86 YA MWAKA 2023**
**HAMADI LYIMO ...................MDAI**
**VERSUS**
**DR. HENRICK BEN MAHENGE............MADAIWA**
**KWA: DR. HENRICK BEN MAHENGE**
**POPOTE ULIPO.**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 02.08. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
ANGALIZO: kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 27 ya mwezi wa JUNI, 2023.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAMWELI BASHAGHEDA SURUMBU** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T299DBD AINA YA TOYOTA NOAH, CHASIS NAMBA SR400224181, ENGINE NAMBA 3S7942814
KWA YEYOTE ATAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.TAARIFA YA POLISI: **MAN/HAN/RB/245097/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**
**Kituo cha NYANKUMBU Mkoa wa GEITA**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 30/2023**
**Jina la Mdai: ROZIMARY MATHIAS**
**Jina la Mdaiwa: MASHESHE DOTTO**
**KUITWA SHAURINI**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: MASHESHE DOTTO - ISAMILO**

**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba TALAKA NA MGAWANYO WA MALI**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 10 Mwezi wa 08 Mwaka 2023 saa 8:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinvyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 26 Mwezi wa 07 Mwaka 2023.

HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE
GEITA.


***OFISI ZA MATANGAZO***
***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mobile: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Marekani yaichukiza China

**BEIJING,** China

CHINA imekosoa vikali uamuzi wa Serikali ya Marekani, kuipatia msaada wa kijeshi Taiwan,


Rais wa Marekani Joe Biden (pichani), aliidhinisha msaada huo wenye thamani ya dola milioni 345, Julai 28 mwaka huu chini ya Mamlaka ya Kutoa Msaada wa Mapato ya Rais (PDA).

Mamlaka hiyo iliyoidhinishwa na Bunge la Congress mwaka jana, inaruhusu Marekani kuhamisha silaha na rasilimali nyingine kutoka katika rasilimali zake za ulinzi.

**Waziri Mkuu wa Taiwan Chen Chien-jen na wizara ya ulinzi na mambo ya nje ya kisiwa hicho, aliishukuru Marekani...**

Msemaji wa masuala ya Kisiwa cha Taiwan katika Serikali ya China, Chen Binhua, alielezea nchi yake inapinga uuzaji wa silaha na kitendo hicho hakitabadilisha nia yake ya kuitaka Taiwan kukamilisha muungano wa kitaifa.

Shirika rasmi la habari la China la Xinhua, liliripoti kwamba Chen pia alikishutumu chama tawala cha Taiwan cha Democratic Progressive Party (DPP) kwa kutumia Marekani kutafuta uhuru wa kisiwa hicho na



kuzidisha hatari ya vita katika mlango wa Bahari wa Taiwan.

Waziri Mkuu wa Taiwan Chen Chien-jen na wizara ya ulinzi na mambo ya nje ya kisiwa hicho,aliishukuru Marekani, lakini hakutoa maoni kuhusu wasiwasi wa China.

Wakati huo huo, bajeti ya baraza la mawaziri la Taiwan kwa mwaka wa 2024, imependekeza ongezeko la asilimia 7.5 la matumizi ya ulinzi hadi karibu dola bilioni 14. **BBC**




Mwanamke raia wa Nigeria akisubiri wateja kununua bidhaa zake pembeni ya barabara. **PICHA: AFP**

## Afrika Kati yapiga kura ya maoni

**BANGUI,** Afrika ya Kati

SHUGHULI ya kuhesabu kura ya maoni inaendelea katika Jamhuri ya Afrika ya Kati baada ya raia kupiga kura kuhusu katiba mpya.

Kura hiyo inalenga kumruhusu Rais Faustin Archange Touadera kugombea kwa muhula wa tatu.

Karibu raia milioni 1.9 walisajiliwa kushiriki kura hiyo inayopendekeza mabadiliko yatakayoongeza mamlaka ya Rais kutoka muhula wa miaka mitano hadi saba na kuondoa ukomo wa mihula miwili.

Mwaka 2020, Touadera alishinda muhula wa pili hadi mwaka 2025, baada ya uchaguzi kuvurugwa na baadhi ya makundi ya waasi, lakini pia ulikabiliwa na madai ya udanganyifu.

Wapinzani wake wanamshutumu kwamba anataka kuwa Rais wa maisha. Matokeo ya mwanzo yanatarajiwa kutolewa baada ya siku nane.

Mahakama ya katiba inatarajiwa kuchapisha matokeo rasmi Agosti 27 mwaka huu. **DW**

## Kenya kupeleka walinda amani nchini Haiti

**PORT-AU-PRINCE**

NCHI ya Haiti imekubali pendekezo la Kenya kuongoza kikosi cha kimataifa cha askari 1,000 kwa ajili ya kuimarisha usalama katika nchi hiyo iliyokumbwa na ghasia

Taarifa ya Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Haiti, Jean Victor Geneus, alisema kuwa Haiti inathamini nia ya mshikamano kutoka nchi hiyo ya Afrika na inatazamia kuukaribisha ujumbe unaopendekezwa na Kenya.

Kenya ilitangaza Jumamosi kuwa ilikuwa tayari kupeleka askari 1,000 wa polisi ili kusaidia kutoa mafunzo na msaada kwa wenzao wa Haiti katika kupambana na magenge ya wahalifu ambayo yamechukua udhibiti wa sehemu kubwa ya mji mkuu, Port-au-Prince.

Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Kenya, Alfred Mutua (pichani), alisema Kenya ingetuma ujumbe wa kutathmini hali ilivyo nchini Haiti katika wiki chache zijazo.

Pendekezo hilo la kuisaidia Haiti bado linatakiwa kukubaliwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na kuidhinishwa na mamlaka za ndani. **DW**



## Watu 44 wauawa katika mlipuko

**BAJAUR,** Pakistan

WATU 44 wameuawa na wengine zaidi ya 100 wamejeruhiwa katika mlipuko uliotokea nchini Pakistan wakati wa maandamano yaliyoandaliwa na chama cha Kiislamu.

Mlipuko huo ulitokea Kaskazini-Magharibi mwa wilaya ya Bajaur, wakati wafuasi wa chama cha Jamiat Ulema-e-Islam-Fazl (JUI-F) wakiandamana kwenda kuhudhuria mkutano.

Polisi waliambia BBC kwamba walipata ushahidi unaoonyesha kuwa mlipuko huo ulikuwa wa shambulio la kujitoa mhanga.

"Shughuli ya uokoaji imekamilika na wote waliojeruhiwa wamepelekwa hospitalini," alisema mkuu wa polisi.

Aidha, alisema huenda idadi ya vifo ikaongezeka zaidi, kutokana na watu 15 kuwa katika hali mbaya.

Sababu ya shambulio hilo bado haijabainika. Vikosi vya usalama vimezingira eneo hilo na uchunguzi kuhusu mlipuko huo unafanyika.

Mamia ya watu walikuwa wakihudhuria mkutano wa wafanyakazi wa JUI-F siku ya Jumapili katika mji wa Khar, katika wilaya ya Bajaurkaribu na mpaka na Afghanistan.

Picha zilionyesha mamia ya watu wakiwa wamekusanyika chini ya dari wakati mlipuko huo ulipotokea karibu na jukwaa.

Mtu mmoja aliyeshuhudia alisema hema hilo liliporomoka na kuwaangukia watu waliokuwa wakijaribu kukimbia. **BBC**

## Putin akubali pendekezo la amani kutoka Afrika

**MOSCOW,** Russia

RAIS wa Russia, Vladimir Putin, amesema nchi yake haipingi kufanya mazungumzo na Ukraine.

Putin (pichani) alisema mpango wa amani uliopendekezwa na Afrika unaweza kutumika kama msingi wa amani, pamoja na ule uliowasilishwa na China.

Hata hivyo, alisema ni vigumu kufanyika kwa mazungumzo hayo kwa sasa kutokana na Ukraine kuendeleza mashambulizi.

Aidha taarifa nyingine zilisema Saudi Arabia inatarajiwa kuwa mwenyeji wa mazungumzo ya kusaka suluhu ya amani yatakayofanyika mwishoni mwa wiki ijayo huko Jeddah.

Vyombo kadhaa vya habari vilisema wajumbe kutoka Ukraine, mataifa ya Magharibi na mengine yanayoendelea watahudhuria, lakini Russia haitashiriki. **DW**



# TEPSI WA AZAM ATUA KMC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC imeinasa saini ya winga wa Azam FC, Tepsi Evance, kwa mkopo wa mwaka mmoja na tayari mchezaji huyo amejiunga na kambi ya timu hiyo.

**Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo, imeeleza kuwa wameingia mkataba wa mwaka mmoja na mchezaji huyo akitokea Azam FC, ikiamini atakuwa msaada mkuba kwenye kikosi hicho.**

"Tuna furaha kuwataarifu kuwa tumeingia mkataba wa mwaka mmoja na Tepsi Evance akitokea Azam FC kwa mkopo," ilieleza taarifa hiyo.

KMC inaonekana kufanya usajili mkubwa kuelekea msimu ujao wa ligi baada ya kutofanya vema msimu uliopita.

Tayari imeshawasajili Rogers Gabriel kutoka Pamba na Juma Shemvuni, Wibol Maseke aliyeachwa na Azam FC, Rahim Shomari na Andrew Sinchimba, ikimtwaa pia straika Ibrahim Elias raia wa Somalia kutoka Klabu ya Kibra United ya Kenya.

Hivi karibuni, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Christina Mwagala, alisema kuwa kimetengwa kiasi cha Sh. bilioni moja kwa ajili ya usajili wa msimu unaokuja na hawatosajili mchezaji yeyote ambaye ameachwa na klabu yake.

"Mkurugenzi wetu mama Hanifa Selemani Hamza, ametenga kiasi cha Sh. bilioni moja kwa ajili ya kufanya usajili, maisha magumu tulioyapitia kwa msimu miwili iliyopita haikuwa rafiki kwetu, lazima tufanye usajili wa maana na kwa pesa hizi KMC hatusubiri wachezaji makapi, sijui nani kaachwa ndiyo tuende kumsajili.

"Msimu huu hatuchukui wachezaji ambao wameshindwa kufanya vizuri walikotoka, badala yake ni wapya kabisa kwenye macho ya mashabiki wa soka nchini na wengine tutawavunjia mikataba kwenye klabu zao na kuwasajili," alisema.

Wakati huo huo, KMC juzi ilicheza mechi ya kujipima nguvu dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro na kushinda mabao 6-4 kwa mikwaju ya penalti, baada ya sare ya bao 1-1 dakika 90 za mchezo.





Timu ya mpira wa miguu ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wakishangilia baada ya kutwaa ubingwa wa michuano ya Maji Cup 2023 kwa kuifunga Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bunda (BUWSSA), mabao 2-1 katika mchezo wa fainali uliopigwa visiwani Zanzibar mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DAWASA mabingwa Maji Cup 2023

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imetwaa ubingwa wa michuano Maji Cup baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya timu ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bunda, BUWSSA.

DAWASA walitwaa ubingwa huo mwishoni mwa wiki katika mchezo wa fainali uliopigwa Uwanja wa Mao Tse Tung visiwani Zanzibar.

Akizungumza baada DAWASA kuibuka na ushindi huo, Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu, aliwapongeza wachezaji wote pamoja na benchi la ufundi kwa jitihada zote walizofanya kuanzia maandalizi ya mashindano hadi kufikia kubeba ubingwa huo.

"Nawapongeza wachezaji wote kwa kuipambania taasisi yetu katika mashindano haya hadi kufikia kuchukua ubingwa huu," alisema Kingu.

Kingu aliongeza kuwa ushirikiano mkubwa pamoja na juhudi za kila mchezaji ni chachu ya mafanikio haya ambapo DAWASA inachukua ubingwa huo kwa mara ya kwanza.

Ushindi huo unaifanya DAWASA inayoonolewa na Kocha Mkuu, Mohamed Magali, kutwaa ubingwa huo kwa mara ya kwanza tangu michuano ya Maji Cup ilipoanzishwa mwaka 2021.

Kocha Mkuu wa DAWASA, Magali, alisema ushirikiano mkubwa kutoka kwa Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kingu pamoja na menejimenti nzima kwa maandalizi mazuri ndiyo siri ya mafanikio hayo.

"Tunaishukuru Menejimenti ya DAWASA inayoongozwa na Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu, Kiula Kingu kwa ushirikiano mkubwa aliyotupa kuanzia maandalizi ya timu, ushiriki wa timu katika mashindano na hatimaye kufanikiwa kuwa mabingwa," alisema Magali.

Mgeni rasmi katika ufunguzi wa fainali za Maji Cup 2023, alikuwa Naibu Waziri Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Shaaban Ali Othman.

Mashindano ya Maji Cup yaliasisiwa mwaka 2021 na hadi sasa huu ni msimu wa tatu yanafanyika yakiwa na kaulimbiu "Thamani ya Maji kwa Uhai na Maendeleo."

## Aisha ang'ara U-18 CECAFA

**Na Saada Akida**

LICHA ya Aisha Mnunka kuonesha kiwango bora kwa kupachika mabao matatu yanayomfanya kuwa kileleni mwa orodha ya wafungaji bora wa michuano ya CECAFA inayoendelea katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wasichana chini ya miaka 18, Bakari Shime, amesema mshambuliaji huyo bado anapaswa kupambana zaidi.

Akizungumza na Nipashe jana, Shime alisema hataki kumpa presha ya kuwa mfungaji bora bali anamsukuma ili kufunga idadi kubwa ya mabao na kuisaidia Tanzania kutwaa ubingwa wa michuano hiyo inayoendelea nchini.

"Asha ni mshambuliaji mzuri, kwa sasa tunamsukuma afunge idadi kubwa ya mabao zaidi kwenye mchezo wetu wa mwisho dhidi ya Uganda. Ushindi katika mchezo huo utatupa uhakika wa kutwaa ubingwa.

"Kwa sasa Tanzania tuna alama tisa, zinazotufanya kuongoza msimamo tukifuatiwa na Uganda yenye pointi sita, wana mchezo mmoja kesho (leo) dhidi ya Burundi, wakishinda mechi hiyo tutakuwa na alama sawa," alisema Shime.

Alisema wanahitaji kufanya vizuri katika mchezo ujao dhidi ya Uganda ambao anaamini utakuwa mgumu kwa sababu ya ubora wa wapinzani wao hao, lakini wamepania kutowapa nafasi ya kushinda.

## Geita Gold yataja malengo 2023/24

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Klabu ya Geita Gold, limesema malengo yao ni kushika nafasi ya tatu kwenye msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2023/24 unaotarajiwa kuanza Agosti 15, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana kutoka mkoani Morogoro ilipo kambi yao, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hemed Morocco, alisema anaendelea kufanya usajili ambao utakwenda kutoa ushindani mkubwa ndani ya kikosi hicho, ili kuweza kutimiza malengo yao.

"Malengo yangu ni kushika nafasi ya tatu msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, hivyo ninahakikisha nasajili wachezaji wenye viwango," alisema Morocco.

Kocha huyo alisema anafurahishwa na ushindani wa namba uliopo ndani ya timu yake kwani kila mchezaji anataka kupata nafasi ya kucheza jambo ambalo linawafanya kuonyesha viwango.

Alisema wiki ijayo wanatarajia kucheza michezo ya kirafiki itakayomsaidia kuangalia ubora na mapungufu ya kila mchezaji.

"Tutaanza kucheza na timu za Ligi Daraja la Kwanza (Championship), halafu baadaye tutakutana na zile za Ligi Kuu, ninaomba mashabiki wetu waendelee kutuamini," alisema.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

## RAYA ATAKIWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich imeanza mazungumzo na Brentford kuhusu mpango wa kumnunua kipa wao, David Raya mwenye umri wa miaka 27, huku mlinda mlango wa Uswisi, Yann Sommer mwenye miaka 34, akijadili kuhamia Inter Milan. ***(Sky Sports)***

## MANE SAFI AL-NASSR

BAYERN Munich pia imekubali ombi la Al-Nassr kumnunua mshambuliaji wa Senegal, Sadio Mane, 31. ***(Fabrizio Romano)***

## KANE, BAYERN KITAELEWEKA

MAAFISA wa Bayern hawatasafiri kwenda London kukutana na wawakilishi wa Tottenham kuhusu mpango wa kumnunua mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 30, lakini klabu hiyo ya Ujerumani bado inawasiliana na Spurs. ***(Sky Sports)***

## SPURS YAMTAKA TEL

TOTTENHAM Hotspur itatumia mazungumzo yao na Bayern kuhusu Harry Kane kujadili nia yao ya kumnunua mshambuliaji wa klabu ya Ujerumani mwenye umri wa miaka, 18 Mathys Tel. ***(Telegraph)***

## LUKAKU KUUZWA JUMLA

CHELSEA imekataa ombi la Juventus la kutaka kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 30, kwa sababu wanataka kumuuza moja kwa moja. ***(Tuttosport)***

## MAXIMIN AUZWA SAUDIA

KLABU ya Newcastle United imemuuza winga Mfaransa, Allan Saint-Maximin mwenye umri wa miaka 26 kwa Al-Ahli ya Saudi Arabia kwa euro milioni 30. ***(Mail)***

## HENDERSON KWENDA FOREST

MANCHESTER United wako tayari kumruhusu mlinda mlango wa England, Dean Henderson mwenye umri wa miaka 26, ajiunge na Nottingham Forest kwa mkopo. ***(Manchester Evening News)***

## VILLA KUMPOTEZEA PEDRO

KLABU ya Aston Villa haitamsajili winga wa Sporting Lisbon na Ureno, Pedro Goncalves mwenye umri wa miaka 25, kwa sababu ofa yao ya juu ya pauni milioni 38.6 ilikuwa pungufu ya bei ya Sporting. ***(Recorg)***

## GALATASARAY NA FRED

KLABU ya Galatasaray inavutiwa na kiungo wa kati wa Manchester United na Brazil, Fred mwenye umri wa miaka 30, lakini kuna pengo katika udhamini kati ya klabu hizo mbili. ***(Sky Sports)***

## FOREST IMEKATAA MZIGO

KLABU ya Nottingham Forest imekataa ombi la rekodi ya klabu la pauni milioni 35 kutoka kwa Brentford kwa ajili ya mshambuliaji wao wa Wales, Brennan Johnson, 22. ***(Telegraph)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# DEMBELE SASA AKARIBIA KUJIUNGA RASMI NA PSG

**PARIS,** Ufaransa

●●● Winga huyo ana kipengele katika mkataba wake ambacho kitamruhusu kuondoka kwa...

OUSMANE Dembele amefikia makubaliano binafsi na Paris Saint-Germain, kuashiria nia yake ya kuondoka Barcelona, duru zimethibitisha kwa 90min.

**Kama ilivyothibitishwa wiki iliyopita, PSG hivi karibuni iliwasiliana na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye ameingia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake pale Camp Nou.**

Barcelona wanataka kumbakisha Dembele na wamefungiwa katika mazungumzo ya mkataba mpya kwa miezi kadhaa, lakini maendeleo bado hayajapatikana.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa anatazamia ongezeko kubwa la mshahara baada ya kukubali kupunguza mshahara wake kwenye mkataba wa muda mfupi aliomwaga wino na Barcelona msimu uliopita wa majira ya joto.

Huku kukiwa hakuna makubaliano yoyote, PSG wamehamisha matumaini ya kumrejesha Dembele kwenye Ligue 1, ambako aling'ara akiwa na Rennes kabla ya kwenda Borussia Dortmund mwaka 2016.

Dembele ana kipengele katika mkataba wake ambacho kitamruhusu kuondoka kwa euro milioni 50.

PSG inaweza kukamilisha usajili wa Dembele kwa kulipa kipengele chakuachiwa kwake, na hilo ni chaguo sasa masharti binafsi yamekubaliwa.

Makubaliano ya mkataba wa miaka mitano yamefikiwa kati ya Dembele na PSG, ambao wameiharifu Barcelona kuhusu hali hiyo.

Klabu hizo mbili zimefanya mazungumzo na jinsi watakavyoendeleza katika saa zijazo itaamua ikiwa PSG itahitaji kulipa kifungu cha kuachiliwa au kufikia makubaliano na Barcelona.

Wakati Barcelona wakitaka Dembele abaki, wao pia wameweka wazi kuwa hawataki kumpoteza bure msimu ujao wa majira ya joto na hivyo kusitasita kufungua mlango wa kuondoka.

Mpango wakiwa Camp Nou ulikuwa ni Barcelona kuachana na mawinga wawili kati ya wanne waandamizi - Dembele, Raphinha, Ansu Fati na Ferran Torres - msimu huu wa majira ya joto.

Hapo awali, Barcelona walitaka kuwatoa Fati na Torres, lakini wote wamekuwa wakisita kuondoka.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,139,8

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 03 AGOSTI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 03/08/23 | 17:00 | Tobol Kostanay vs FC Basel | 3.10 | 3.40 | 2.16 |
| 02. 03/08/23 | 18:00 | Pyunik Yerevan vs Kalmar | 2.31 | 3.25 | 2.95 |
| 03. 03/08/23 | 18:00 | Santa Coloma vs Sutjeska | 2.80 | 3.40 | 2.33 |
| 04. 03/08/23 | 19:00 | Urartu vs Farul Constanta | 2.51 | 3.21 | 2.71 |
| 05. 03/08/23 | 19:00 | FK Panevezys vs Hapoel Beer Sheva | 3.06 | 3.36 | 2.20 |
| 06. 03/08/23 | 19:45 | Zalaegerszegi TE vs NK Osijek | 2.51 | 3.27 | 2.66 |
| 07. 03/08/23 | 20:00 | Sepsi Osk vs CSKA Sofia | 2.71 | 3.21 | 2.51 |
| 08. 03/08/23 | 20:00 | Dila Gori vs Vorskla Poltava | 2.35 | 3.35 | 2.80 |
| 09. 03/08/23 | 21:00 | Vojvodina vs Apoel Nicosia | 2.75 | 3.25 | 2.44 |
| 10. 03/08/23 | 21:00 | Aarhus vs Brugge | 3.10 | 3.25 | 2.22 |
| 11. 03/08/23 | 21:30 | Larne vs KF Ballkani | 2.65 | 3.39 | 2.46 |
| 12. 03/08/23 | 21:45 | FC Luzern vs Djurgardens IF | 2.11 | 3.40 | 3.20 |
| 13. 03/08/23 | 22:00 | Shamrock Rovers vs Ferencvaros TC | 3.05 | 3.30 | 2.23 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CHELSEA YAPUUZA MKOPO WA ROMELU




**TURUN,** Italia

CHELSEA wamefuta uchunguzi kutoka kwa Juventus kuhusu mkataba wa mkopo wa mshambuliaji Romelu Lukaku, kwa mujibu wa '90min'

Lukaku amerejea hivi punde kutoka kwenye mkataba wa mkopo na Inter na anatarajiwa kuondoka Chelsea wiki chache zijazo baada ya kuachwa nje ya kikosi cha Mauricio Pochettino kwa ajili ya ziara ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani.

Inter walikuwa wakiongoza mbio za kuinasa saini yake, lakini kwa mshtuko waliachana na harakati za muda mrefu za kumnasa mshambuliaji huyo, huku kukiwa na tuhuma kwamba amekuwa akifanya mazungumzo na Juventus, licha ya Lukaku kudai kwa faragha na hadharani kwamba hatawahi kuhamia timu nyingine ya Italia.

Mchezaji mwenzake wa zamani wa Inter Lautaro Martinez hivi majuzi alikiri kuwa 'amesikitishwa' na tabia ya Lukaku msimu huu wa majira ya joto.



## Eriksen asifia usajili wa Hojlun

**MANCHESTER,** England

CHRISTIAN Eriksen amefurahishwa na maendeleo ya mwenzake Rasmus Hojlund kwa mwaka jana na anaamini kuwa Manchester United inasajili "mchezaji mzuri sana".

Baada ya kufanikisha mikataba ya kiungo Mason Mount na kipa mahiri Andre Onana, waliongeza umakini wao katika kusajili mshambuliaji mpya.

United imekuwa ikihusishwa mara kwa mara na mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane, lakini wakaishia kumtafuta mshambuliaji wa Atalanta anayekuja kwa kasi, Hojlund.

Klabu hizo zimekubali mkataba wenye thamani ya pauni milioni 64 pamoja na nyongeza ya pauni milioni nane kwa ajili ya mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ambaye amemvutia mchezaji mwenzake wa Denmark, Eriksen.

"Ni nini yeye? Yeye ni namba tisa mwenye nguvu," kiungo huyo wa United aliliambia Shirika la Habari la PA.

"Amekua sana katika mwaka uliopita tangu nilipomwona kwa mara ya kwanza na timu ya taifa hadi mwaka mmoja, kwa hivyo ni mchezaji mzuri sana."

"Ni mtu mzuri, ni mche
mzuri. Kama nilivyose
amekua, akigeuka kuwa
tu, ambayo ameichezea t
ya taifa.

"Lazima niwe mkweli
ona mechi nyingi kama
kwa Atalanta, lakini n
jinsi wanavyocheza na a
gia vizuri huko, kwa hivy
mchezaji mzuri."

Hojlund aliichezea FC
penhagen na Sturm Gra
Austria kabla ya kujiunga
Atalanta msimu uliopita
majira ya joto, akifunga
bao tisa kwenye Serie A
pia sita katika mechi ny
alizochezea Denmark.



359,317/-

# CAF YACHELEWESHA RATIBA LIGI KUU BARA

**Na Abdallah Mataka**

KUCHELEWA kutoka kwa ratiba ya Ligi Kuu Tanzania Bara hadi sasa kumetokana na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kuchelewesha ratiba ya mashindano mapya ya African Football League (Super Cup), imeelezwa.

Tayari ya Bodi ya Ligi nchini (TPLB), imeeleza kuwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/24, itaanza rasmi Agosti 15, mwaka huu, lakini bado haijatangaza ratiba ya ligi hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu TPLB, Almasi Kasongo, alisema ratiba kwa mashindano yote ambayo yalikuwa tangu hapo nyuma kila kitu kimekaa vizuri, yakiwamo Mapinduzi Cup, kuwania kufuzu CHAN na mengineyo.

"Nina uhakika kabisa mpaka itakapofika wiki ijayo, tutakuwa tumekamilisha hilo zoezi na kuweza kutangaza ratiba yetu ya msimu wa 2023/24," alisema Kasongo.

"Kama unavyojua ratiba ya Ligi Kuu inaakisi na mshindano mengine, kama Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho ambalo tayari CAF wameshatoa ratiba yake, lakini sasa imeongezeka African Super Cup na moja ya timu shiriki ni Klabu ya Simba," alisema Kasongo na kuongeza:

"Mpaka sasa Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), halijatoa ratiba kamili zaidi imetaja tu tarehe ya ufunguzi wa mashindano hayo na mechi itachezwa wapi, lakini kwa maana ya ratiba nzima bado hawajaitangaza na unaona jinsi wanavyokwamisha zoezi zima la ratiba yetu kuweza kuakisi ratiba ya mashindano hayo.

"Hatujui hata mashindano hayo yanachezwaje, imetaja tu itafanyika kati ya mwezi wa 10 na 11, hivyo inachezwaje bado ni kitendawili."



AFCON 2027... Timu ya wakaguzi kutoka Shirikisho la Soka Afrika (CAF) ya utayari wa nchi za Kenya, Uganda na Tanzania kuwa wenyeji AFCON 2027, ikifanya ukaguzi katika Uwanja wa Amaan mjini Zanzibar jana na baadaye Hospitali ya Mnazi Mmoja visiwani humo. Kushoto rais wa Shirikisho la Soka nchini, Wallace Karia. **MPIGAPICHA WETU**

## Robertinho apagawa

INATOKA UKURASA 24

ya kuchapwa bao 1-0 mechi ya pili jioni, zote zikichezwa Uwanja wa Soguksu Spor Kompleksi.

Kuelekea Simba Day, Simba imeendelea kufanya shughuli mbalimbali za kijamii na jana walitembea shule ya watoto wenye ulemavu wa akili, Sinza Kinondoni kwa kutoa mahitaji muhimu ikiwamo vyakula na maji.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema wiki hii wanaendelea kurejesha kwa jamii kama ilivyokuwa mwaka jana walitembelea kambi ya wazee Nunge Kigamboni na mwaka huu wameenda Sinda kwa ajili ya watoto hao.

"Shule ina watoto 91 kupitia shughuli hii tunaamini watu watafahamu kuhusu kituo hiki. Tunawapongeza sana walimu kwa kazi hii kwani ni kazi zaidi ya kujitolea hata kama mnalipwa, lakini mnajitoa sana na malipo zaidi ni kwa Mungu.

"Lakini nawapa hongera kwa wazazi waliona umuhimu wa kuleta watoto shuleni, hili ni jambo jema kwani wameamua kupambana na watoto wao," alisema Ahmed.

Naye Mkuu wa shule hiyo, Catherine Msese , ameishukuru Klabu ya Simba kwa kuwakumbuka na kuiomba iwe balozi wao kwani watoto hao wanapenda pia michezo.

"Nipende kuwashukuru Simba kwa kututembelea hapa ni jambo la faraja, ombi langu kwa Simba naomba muwe mabalozi wetu kwani watoto hawa wanapenda michezo ambayo ni afya na inawajenga. Watu hawaelewi watoto wenye ulemavu wa akili wanaweza kubadilika wanapopelekwa shule kama watoto wengine, " alisema Msese.

## *Mayele: Nitarudi*

INATOKA UKURASA 24

kuongeza dau, lakini ilifika mwisho wakanyanyua mikono kutokana na timu zilivyokuwa zikipanda kila wao wanavyotaka kumbakisha.

Alikiri kuwa klabu za Afrika Kaskazini maarufu kama za Waarabu hazishindwi kuchukua mchezaji yeyote chini ya Jangwa la Sahara kutokana na kuwa vizuri zaidi kiuchumi.

"Ilikuwa vita, sisi tukipanda dau la usajili na mshahara na wenzetu pia wanapanda, imekwenda hivyo mpaka tukashindwa, hizi timu za Afrika Kaskazini zina uchumi mkubwa zikitaka mchezaji hazishindwi kumpata," alisema Ngai.

Alisema si Pyramids tu ilikuwa ikimhitaji bali zilikuwapo zingine ikiwamo moja kutoka nchini Qatar, lakini Mayele mwenyewe alichagua kwenda Misri kwa sababu anaamini kuna ushindani na ligi bora.

Mayele alitambulishwa rasmi juzi usiku kuwa mchezaji wa klabu hiyo nchini Misri ambayo msimu uliomalizika ilifika robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/08/23 | 13:00 | Urawa Red Diamonds vs Yokohama Marinos | 2.23 | 3.35 | 2.70 |
| 02. 06/08/23 | 13:00 | Kyoto Sanga FC vs Kashiwa Reysol | 2.22 | 3.05 | 2.90 |
| 03. 06/08/23 | 13:00 | Sagan Tosu vs Avispa Fukuoka | 2.40 | 3.00 | 2.70 |
| 04. 06/08/23 | 13:00 | Thespakusatsu vs Tochigi SC | 2.75 | 2.90 | 2.45 |
| 05. 06/08/23 | 13:00 | Omiya Ardija vs Blaublitz Akita | 2.65 | 2.95 | 2.46 |
| 06. 06/08/23 | 13:00 | Tokushima Vortis vs JEF United Ichihara Chiba | 2.85 | 3.05 | 2.27 |
| 07. 06/08/23 | 14:30 | Karlsruher SC vs Hamburger SV | 2.90 | 3.70 | 2.16 |
| 08. 06/08/23 | 14:30 | 1 FC Nuremberg vs Hannover 96 | 2.16 | 3.55 | 3.00 |
| 09. 06/08/23 | 14:30 | RSC Anderlecht vs Royal Antwerp FC | 2.41 | 3.45 | 2.65 |
| 10. 06/08/23 | 16:00 | Kalmar FF vs AIK | 2.55 | 3.00 | 2.55 |
| 11. 06/08/23 | 16:00 | FK Teplice vs FK Jablonec | 2.60 | 3.20 | 2.37 |
| 12. 06/08/23 | 17:30 | Grasshopper Club Zurich vs FC Basel 1893 | 2.75 | 3.45 | 2.16 |
| 13. 06/08/23 | 18:00 | FK Haugesund vs Rosenborg BK | 2.75 | 3.25 | 2.23 |
| 14. 06/08/23 | 18:00 | Tromsoe IL vs Lillestrom SK | 2.27 | 3.25 | 2.70 |
| 15. 06/08/23 | 18:00 | Blau-Weiss Linz vs TSV Hartberg | 2.39 | 3.25 | 2.55 |
| 16. 06/08/23 | 19:00 | Sunderland AFC vs Ipswich Town | 2.46 | 3.30 | 2.70 |
| 17. 06/08/23 | 20:15 | KV Kortrijk vs St. Truidense VV | 2.80 | 3.40 | 2.33 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 01/08/2023


| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2531 | Paris St Germain vs Inter | 1.83 | 3.56 | 3.66 |
| 14:00 | 1552 | Heidenheim vs Pafos FC | 1.47 | 4.10 | 5.20 |
| 14:00 | 3048 | China W vs England W | 6.95 | 4.04 | 1.41 |
| 14:00 | 3710 | Haiti W vs Denmark W | 8.76 | 4.69 | 1.29 |
| 17:00 | 3444 | Mainz vs St. Gallen | 1.45 | 4.48 | 5.29 |
| 18:00 | 3580 | Valmiera Fk/Bjss vs Tre Penne Galazzano | 1.15 | 7.20 | 14.00 |
| 18:00 | 4711 | St.polten Spratzern W vs Gyori Eto W | 1.46 | 4.59 | 5.10 |
| 20:00 | 5753 | Kvarnsvedens IK vs IFK Osteraakers FK | 5.31 | 4.50 | 1.45 |
| 20:30 | 1845 | Balzan Youths vs Neman Grodno | 2.85 | 3.30 | 2.34 |
| 20:30 | 2120 | Panathinaikos vs SC Dnipro 1 | 1.54 | 4.05 | 5.14 |
| 20:30 | 3983 | Zimbru vs Fenerbahce | 10.72 | 5.89 | 1.22 |
| 21:00 | 4988 | Olimpija Ljubljana vs Ludogorets Razgrad | 3.26 | 3.21 | 2.12 |
| 21:00 | 5321 | BATE Borisov vs Aris Limassol | 3.91 | 3.51 | 1.82 |
| 21:00 | 5349 | Swift Hesperange vs The New Saints | 1.68 | 3.80 | 4.50 |
| 21:30 | 2010 | Slovan Bratislava vs Zrinjski Mostar | 1.89 | 3.26 | 3.95 |
| 21:30 | 2563 | St Mirren B vs Albion Rovers | 2.65 | 3.87 | 2.15 |
| 21:30 | 3168 | Brechin City vs Heart of Midlothian B | 1.62 | 3.63 | 4.80 |
| 21:30 | 5288 | Elgin City vs St Johnstone B | 1.62 | 3.63 | 4.80 |
| 21:45 | 1401 | Radcliffe Borough vs Halifax | 3.32 | 4.08 | 1.81 |
| 21:45 | 1684 | Kilmarnock FC B vs Bonnyrigg Rose | 2.53 | 3.93 | 2.22 |
| 21:45 | 2300 | Spartans FC vs Glasgow Rangers FC B | 2.48 | 4.03 | 2.23 |
| 21:45 | 4207 | Partizani Tirana vs Atletic Club Escaldes | 1.17 | 6.63 | 14.06 |
| 21:45 | 4959 | Bishop Stortford vs Leyton Orient | 4.10 | 3.90 | 1.62 |
| 21:45 | 5594 | Tranent Juniors vs Motherwell B | 2.16 | 3.73 | 2.71 |
| 22:00 | 1513 | Buducnost vs FC Struga Trim Lum | 2.30 | 3.25 | 2.95 |
| 22:15 | 3388 | Afturelding Mosfellsbaer W vs Grindavik W | 1.91 | 3.90 | 2.95 |
| 23:00 | 1952 | Deportivo Municipal vs Asociacion Deportiva Tarma | 2.35 | 3.16 | 2.71 |
| 23:00 | 3299 | Manta vs America | 1.63 | 3.46 | 5.09 |

### JUMATANO - 02/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:00 | 2185 | Libertad Asuncion vs Fortaleza CE | 2.16 | 3.16 | 3.11 |
| 01:00 | 3465 | Argentinos Juniors vs Fluminense | 2.29 | 3.04 | 2.99 |
| 01:00 | 4202 | Sampaio MA vs Botafogo SP | 2.17 | 2.99 | 3.29 |
| 03:00 | 1640 | River Plate vs Internacional | 1.47 | 3.94 | 6.10 |
| 03:00 | 5378 | Bolivar vs Atletico Pr | 1.86 | 3.44 | 3.69 |
| 03:00 | 5677 | SC Emelec vs Defensa Justicia | 2.19 | 3.17 | 3.06 |
| 03:30 | 3249 | Leones FC vs Deportes Quindio | 2.15 | 3.15 | 3.15 |
| 03:30 | 3697 | Corinthians vs NewellS Old Boys | 2.00 | 3.01 | 3.73 |
| 06:00 | 1188 | AC Milan vs Barcelona | 3.65 | 3.71 | 1.80 |
| 10:00 | 4724 | South Africa W vs Italy W | 4.68 | 3.72 | 1.62 |
| 10:00 | 5168 | Argentina W vs Sweden W | 5.71 | 3.88 | 1.50 |
| 12:30 | 2394 | Machida Zelvia vs Niigata Albirex | 2.35 | 3.30 | 2.69 |
| 13:00 | 1251 | Nagoya Grampus vs Urawa Red Diamonds | 2.60 | 3.11 | 2.55 |
| 13:00 | 1264 | Kashiwa Reysol vs Consadole Sapporo | 2.80 | 3.46 | 2.21 |
| 13:00 | 1732 | Ventforet Kofu vs Vissel Kobe | 3.77 | 3.57 | 1.80 |
| 13:00 | 1856 | FC Tokyo vs Roasso Kumamoto | 2.15 | 3.21 | 3.10 |
| 13:00 | 4274 | Jamaica W vs Brazil W | 11.24 | 5.52 | 1.21 |
| 13:00 | 4615 | Kawasaki Frontale vs Kochi United SC | 1.24 | 5.48 | 9.13 |
| 13:00 | 5282 | Panama W vs France W | 20.33 | 9.55 | 1.06 |
| 13:00 | 5538 | Tochigi SC vs Avispa Fukuoka | 3.11 | 3.21 | 2.14 |
| 13:00 | 5948 | Cerezo Osaka vs Shonan Bellmare | 1.75 | 3.56 | 4.02 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumanne Agosti 1, 2023
Nipashe




Chelsea yapuuza mkopo wa Lukaku UKURASA 22

TUPO PAMOJA...



Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, akimkadidhi Mkuu wa Shule ya Watoto wenye Ulemavu wa Akili Sinza, Catherine Msese, misaada na mahitaji mbalimbali ikiwamo juisi na maji, ikiwa ni moja ya shughuli zao wanazozifanya kurejesha kwa jamii katika Wiki ya Simba kuelekea Simba Day Agosti 6, mwaka huu. Makabidhiano hayo yalifanyika shuleni hapo, Sinza, Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Mayele: Nitarudi Yanga

## Aaga kwa uchungu akisimulia ilivyokuwa vigumu kuondoka, huku akichambua usajili...

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA Fiston Mayele ametambulishwa rasmi na Klabu yake mpya ya Pyramids ya Misri, huku akiwaaga wanachama na mashabiki wa Yanga kwa uchungu akisema ipo siku isiyo na jina anaweza kurudia tena kwenye kikosi hicho na kuwatakiwa kila la kheri kwenye msimu mpya wa mashindano yajayo.

**Akiwaaga wanachama na mashabiki wa Yanga, Mayele alisema ana imani bila yeye, Yanga inaweza kufanya vema kwani wamesajili wachezaji wazuri, lakini akikumbuka mazuri yote, mafanikio na nyakati za furaha walizokuwa nazo pamoja.**

"Leo nataka nitoe shukrani zangu, maamuzi niliyoyachukua ni magumu, lakini sina jinsi ya kufanya, nimekuja hapa mmenipokea vizuri nilikuwa naishi kama kwetu tu Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, natoa taarifa kwamba nakwenda kutafuta changamoto nyingine.

"Nimekaa sana kwenye vikao na viongozi, wamepambana sana kutaka kunibakisha, wametumia kila aina ya uwezo wao kunishawishi nibaki, lakini na mimi nikawaambia waniruhusu tu niende kutafuta changamoto nyingine nje ya hapa, najua Yanga ni nyumbani, kuna leo, kesho na keshokutwa naweza kurudi kwa sababu hii imeshakuwa ni familia yangu na wao hawawezi kuniacha," alisema mchezaji huyo ambaye mbali na kuwa straika namba moja wa timu hiyo, lakini alikuwa maarufu kutokana na aina yake ya ushangiliaji iliyopendwa na wengi.

Mayele pia alikumbushia nyakati ambazo zilikuwa za furaha kwa wanachama na mashabiki ambazo zitamfanya kuikumbuka klabu hiyo na watu wake kwa ujumla.

"Natoa shukrani zangu za dhati kwa Klabu ya Yanga kwa sababu tulikuwa wote kwa misimu miwili ambayo ilikuwa mizuri sana, tulifurahi sana, tumechukua mataji sita kwa misimu hiyo na tumeweza kupeleka timu fainali ya Kombe la Shirikisho la Afrika na tumepambana kweli kweli pamoja na viongozi, benchi la ufundi, wanachama na mashabiki pia, nakumbuka mechi dhidi ya US Monastir mvua ilinyesha kweli, lakini mashabiki walijaa uwanjani na tukashinda," alisema.

Aidha, alikiri kuwa kulikuwa na baadhi ya nyakati ngumu, lakini viongozi wa klabu hiyo wakiongozwa na rais wa Klabu, Injinia Hersi Said, walikuwa karibu nao kutatua changamoto yoyote, akimtaja rais huyo kuwa alikuwa nao muda wote na sehemu zote wanazokwenda.

Naye Mjumbe wa Kamati ya Utendaji wa klabu hiyo, Alex Ngai, alisema viongozi wa Yanga walifanya kila njia ikiwamo

INAENDELEA UKURASA 23

# Robertinho apagawa na samba la nyota wake

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

BAADA ya ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Batman Petrol Spor ya Uturuki juzi kwenye Uwanja wa Soguksu Spor Kompleksi nchini humo, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, ameonesha kuridhika na kiwango cha wachezaji wake, akisema kwa sasa wanaiweza staili ya samba ambayo amekuwa akiwafundisha.

Robertinho alisema amekunwa mno na kiwango kilichooneshwa zaidi kipindi cha pili kwenye mechi hiyo ambacho ndicho kilichotoa matokeo ya ushindi.

"Nimeridhishwa na kiwango cha kipindi cha pili kwa sababu tulibadilisha matokeo pia kwa sababu hadi mapumziko tulikuwa bao 1-1, nina furaha kwa sababu haikuwa rahisi kwa kuwa wapinzani wetu walicheza vema, ni timu ngumu na wakati mwingine walicheza kwa nguvu ingawa ilikuwa ni hatari kwetu lakini ni nzuri kwa sababu ni kipimo kizuri kwetu tutakapokutana na timu za aina hiyo huko mbele.

"Nina furaha tumetumia mifumo mbalimbali, ikiwamo samba ambayo waimetendea haki, kucheza bila mpira, kutengeneza nafasi, viungo wa kati wamecheza vema," alisema.

Kocha huyo raia wa Brazil alisema anajua ana mashindano mengi makubwa na magumu, hivyo anawatengeneza wachezaji wake ili waweze kukabiliana na mechi hizo kwenye mazingira yoyote na timu yoyote hata iwe kubwa na ngumu kiasi gani.

"Naona hata kwenye fiziki wako vizuri, labda kidogo hawa waliochelewa kuingia kambini, lakini nalo litaisha hivi karibuni," alisema.

Simba imemaliza kambi yao nchini Uturuki na inatarajia kurejea kati ya leo na kesho kwa ajili ya kujiandaa na Tamasha la Simba Day Agosti 6, mwaka huu ambapo itacheza dhidi ya Power Dynamos ya Zambia.

Ikiwa Uturuki, imecheza mechi nne dhidi ya Zira FC ya Azerbaijani na kutoka sare ya bao 1-1 Julai 24, na Alhamisi iliyopita ikicheza asubuhi mechi dhidi ya Turan Tovuz pia ya nchini humo na kushinda mabao 2-0, kabla

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >